SportPesa
TZS. 1,119,012,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

## SWEDEN yapongeza Tanzania uhuru wa habari, demokrasia





# Nipashe

Jumamosi Aprili 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580910

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## UGUMU WA MAISHA

# Wabunge wataka mkakati wa kuwanusuru wananchi

**MFUMO** uagizaji petroli waibua mvutano, tozo mafuta ya kula, Spika atoa maagizo maalum ...*Endelea Ukurasa 2 & 3*



Rais Samia Suluhu Hassan, akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa Nembo ya Sensa ya Watu na Makazi, mjini Zanzibar jana, itakayofanyika Agosti 23 nchi nzima. Kushoto ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia akemea mila na fikra potofu kuhusu sensa

UKURASA 2

## Moto waibuka tena Karume wateketeza maduka machinga

UKURASA 3



Mmoja wa wafanyabiashara katika Soko la mabegi Ilala Karume, jijini Dar es Saaam akimwaga maji kuzima moto uliounguza eneo la soko hilo, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

MICHEZO KOCHA AL AHLY AIONYA ORLANDO KWA SIMBA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (kulia), akikabidhi Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald Wright, baada ya mazungumzo yao katika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ADAM MZEE**

# Wabunge wataka mkakati kuwanusuru wananchi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kuweka mkakati wa kunusuru ugumu wa maisha unaotokana na kupanda kwa bei za mafuta nchini.

Hoja hiyo iliibuka jana bungeni jijini hapa wakati watunga sheria hao walipokuwa wanachangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka ujao wa fedha.

Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo (CCM), alisema kwa sasa hali ni mbaya kwa wananchi kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa, akipendekeza kwamba katika hali kama hiyo, serikali inatakiwa kuandaa mkakati wa kuwanusuru wananchi.

"Serikali inatakiwa kuchukua hatua za makusudi kunusuru hali mbaya waliyonayo wananchi kwa kuwapunguzia adha hiyo ya kupanda kwa bei ya bidhaa," alisema.

Prof. Mkumbo alisema bidhaa zimepanda bei kutokana na kupanda kwa mafuta kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea kwa muda mrefu.

"Inatakiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja Kamati ya Bajeti wakae na kufikiria kuchukua hatua za kupunguza adha ya kupanda kwa bei ya bidhaa kwa wananchi.

"Serikali inaweza kuondoa tozo ya Sh. 792 kwenye mafuta, wanaweza kuziahirisha tozo hadi Julai au Agosti na kuzirudisha baada ya hali kukaa vizuri," alisema.

Prof. Mkumbo alifafanua kuwa tozo zinazopungua, zinaweza kufidiwa kwa serikali kukopa kutoka nje kwa kuwa nchi haipo katika hali nzuri, hivyo ni vyema kunusuru hali hiyo.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba (CCM), alisema kuwa katika kukabiliana na makali ya maisha kwa wananchi, serikali iwaruhusu wananchi kutumia mabati ya geji 40 ambayo ni ya bei rahisi badala ya 'kuyapiga vita' na kuwataka watumie ya geji za juu.

Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei (CCM), alisema mfumuko wa bei ya mafuta ni wa dunia nzima na ni mkubwa tangu mwaka 1982, hivyo nchi haiwezi kuutatua kwa kuwa hautoki ndani ya nchi.

"Kama nchi hatuwezi kuepuka mfumuko huo kwa sababu si wetu, utatuzi wake si wa haraka na wala si wa benki kuu, kinachotakiwa ni kutafuta namna bora ya kukabiliana nao," alishauri.

Mbunge wa Mbogwe mkoani Geita, Nicodemus Maganga (CCM), alisema ugumu wa maisha ni kilio kinachosikika mitaani kwa sasa kutokana na kupaa kwa bei ya mafuta.

"Kuna vyombo vya serikali vinachangia kumuumiza mwananchi. Mfano, kuna masharti magumu kufungua kituo cha mafuta huko kijijini, hadi sasa kule kwangu wananunua petroli Sh. 5000 kwa lita kwenye vidumu, Sh. 3,000 ni kwenye vituo," alisema.

**UHABA MAFUTA YA KULA**

Mbunge wa Mafinga, Cosato Chami (CCM), alisema kwamba ili kukabiliana na kupanda kwa bei ya bidhaa, nchi inatakiwa kujitosheleza kwa bidhaa nyingi kama mafuta na sukari na kama utaratibu huo ungezingatiwa, nyakati kama hizi hali zisingekuwa ngumu kwa wananchi.

"Lakini pia wakati kama huu majeshi yanaweza kutumika kuzalisha mazao, na mwakani nchi ingekuwa na bidhaa za kutosha kama karanga, ufuta na mazao mengine yanayozalisha mafuta," alisema.

Mbunge wa Igunga, Nicolaus Ngassa (CCM), aliitaka serikali kuutazama upya uamuzi wake wa kuongeza tozo kwenye mafuta ya kula yanayoingizwa kutoka nje ya nchi, akisisitiza kuwa ndicho chanzo cha kupaa kwa bei ya bidhaa hiyo nchini.

"Kwa sasa tuna tatizo la uhaba wa mafuta kwa sababu uzalishaji wa ndani umeyumba, viwanda vimekosa malighafi, vimesimama.

"Tumeweka zuio la mafuta ya nje kwa kuweka tozo kubwa kwa lengo la kulinda soko la ndani, lakini uzalishaji wetu umeshindwa kukidhi mahitaji ya soko la ndani. Tuangalie vizuri suala hili ili kutowaumiza zaidi wananchi," alishauri.

Mbunge huyo pia aliitaka serikali kutatua tatizo la uhaba wa wakaguzi wa ndani katika maeneo mbalimbali, pia kuhakikisha masoko kwa ajili ya machinga yanajengwa ndani ya mji, siyo nje ya mji.

Mbunge wa Buchosa, Eric Shigongo (CCM), alisema wakulima ambao ni asilimia 65 hadi 70 ya Watanzania, wana umaskini mkubwa, hivyo wanatakiwa kuwezeshwa ili wawe na maisha yenye unafuu.

**MVUTANO UAGIZAJI PETROLI**

Mbunge wa Geita, Joseph Musukuma (CCM), alisema kuna haja serikali kuja na bajeti ya nyongeza kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na kuweka mfumo wa ruzuku katika biashara ya mafuta.

Pia alishauri kufanyike mabadiliko ya matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama barabara na maji, zielekezwe kwenye ununuzi wa mafuta huku akiukosoa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja, akisisitiza serikali iruhusu wafanyabiashara waagize mafuta wenyewe badala ya kuagiza kwa pamoja.

Mbunge wa Msalala mkoani Shinyanga, Idd Kassim, alisema ni hatari Tanzania kurudi kwenye uagizaji huria wa mafuta, akisisitiza kuwa unahatarisha usalama wa nchi, hasa kipindi hiki cha msuguano kati ya Ukraine na Russia.

Alisema njia nzuri ya kukabiliana na kupaa kwa bei ya nishati hiyo ni kupunguza baadhi ya tozo za serikali, jambo ambalo Mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby alisisitiza bungeni Jumatano kwamba haliwezani kwa kuwa serikali itashindwa kutekeleza mambo mengi ikiwamo ulipaji wa mishahara ya watumishi wa umma.

Mbunge Kassim pia alitaka serikali kuongeza fungu kwa ajili ya ukarabati wa barabara za vijijini ambazo alidokeza kuwa nyingi zina hali mbaya, pia kuimarisha usimamizi wa fedha za ukarabati wa barabara hizo.

# Samia akemea mila potofu kwenye sensa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan jana alizindua nembo ya Sensa ya Watu na Makazi huku akitaka elimu itolewe ili kufanikisha jambo hilo kuondoa fikra potofu katika jamii.

Sambamba na uzinduzi huo, Rais alitangaza rasmi kuwa sensa hiyo ya watu na makazi itaanza rasmi Agosti 23, mwaka huu.

Pamoja na uzinduzi huo, alisema ili kazi hiyo ifanikiwe, lazima elimu kwa jamii itolewe kuhusu umuhimu wa sensa na watu kukubali kuhesabiwa.

Uzinduzi wa nembo hiyo na kutangazwa rasmi kwa tarehe ya kuanza sensa, ulifanyika katika hoteli ya Golden Tulip, pembezoni mwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Zanzibar.

Alisema kuna baadhi ya watu wanaoamini kuhesabiwa ni balaa, nuksi na hasadi, hivyo ni vyema elimu itolewe ili kubadili mitazamo hiyo hasi.

Pia alisema kuwa baadhi ya watu katika jamii huwaficha baadhi ya watu wakiwamo wenye ulemavu wakati wa sensa, hivyo kusisitiza kuwa jambo hilo halikubaliki na kwamba kila Mtanzania aliye hai anapaswa kuhesabiwa ili kupata huduma muhimu na serikali kupanga mipango ya maendeleo.

"Mwende mkatoe elimu kwa jamii ili kila mmoja afahamu kwamba tunahesabiwa kwa ajili ya kuweka sawa hesabu zetu za maendeleo au huduma za maendeleo na kiuchumi. Hakuna sababu nyingine iliyojificha nyuma ya pazia," alisema.

Alisema serikali haiwezi kupanga mipango yake ya maendeleo bila kuwa na takwimu sahihi kwa watu wake wote, hivyo ni lazima kuwa na hesabu ili kujipanga vizuri kwa maendeleo.

Rais alisema kwa mujibu wa miongozo na mapendekezo ya Umoja wa Mataifa, kila nchi inatakiwa kufanya sensa kila baada ya miaka 10 kwa kutegemeana na uchumi wa nchi husika ikiwa na lengo la kufanya ulinganishi kati ya sensa moja hadi nyingine.

Alisema uzinduzi huo ni kutimiza vigezo vya umoja huo katika mpango mkakati wa nchi wanachama kufanya sensa ya watu na makazi katika mzunguko wa miaka 10 na kwamba Tanzania iko ndani ya mzunguko huo.

Pia alisema sensa ya watu na makazi kwa Tanzania si jambo geni kufanyika na tangu kuasisiwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa zimeshafanyika sensa tano katika miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002,2012 na sasa 2022.

Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, alisema nguvu kazi ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa lolote na Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alisema nchi ina maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini na kwamba ili nchi iendeee inahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

"Ukichambua mafundisho hayo, ni dhahiri kwamba changamoto kubwa za kimaendeleo na nyenzo za kuzitatua zinahusu watu na makazi," alisema.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema matokeo ya sensa hutumika kama rejea kwenye kutunga sera na mipango ya kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Kwa upande wake, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema serikali zote mbili zinahitaji kujua idadi ya watu katika kila familia na maeneo ya utawala ili kuimarisha utoaji wa huduma za jamii na ujenzi wa miundombinu.

Alisema utekelezaji wa dhamira ya uendeshaji wa uchumi kwa njia ya kijiditali, unahitaji kuwa na takwimu sahihi za watu, makazi na shughuli wanazozifanya na kwamba utumiaji wa takwimu kupitia njia ya kisasa utarahisisha utekelezaji wa mipango katika ukusanyaji wa mapato, mifumo jumuishi ya kifedha, bima na mawasiliano bora ya simu na mitandao.

HABARI KITAIFA

# Moto waibuka tena soko Karume, wateketeza mabanda ya machinga

**Na Maulid Mmbaga**

VIBANDA 33 vya biashara vikiwa na bidhaa mbalimbali katika soko la Karume, jijini Dar es Salaam, vimeteketea moto chanzo kikidaiwa kuwa ni uunganishwaji wa umeme kinyume cha taratibu.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, aliwaambia waandishi wa habari baada ya kuona athari zilizosababishwa na moto huo kuwa moto huo uliunguza upande wa mabanda ya wenye ulemavu saa 11:00 alifajiri.

Alisema kutokana na tukio hilo, ofisi yake itaunda kamati ya uchunguzi ambayo itafanya kazi kwa siku tano na kutoa taarifa ili kuwaruhusu wafanyabiashara hao waendelee na shuhuli na kurudi katika hali yao ya kawaida.

"Ziko taarifa kuwa kuna mwananchi ambaye alikuwa anawaunganishia umeme wafanyabiashara hawa kinyume cha utarabibu, kwa hiyo niagize Jeshi la Polisi asakwe au yeye mwenyewe ajisalimishe kwa polisi haraka iwezekanavyo.

"Sisi tunajua kwa mujibu wa sheria kazi hiyo inatakiwa ifanywe na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) sasa tunavyokuwa tuna mtu naye anajigeuza kuwa hao ni kinyume cha utaratibu. Lakini nimshukuru mwenyekiti wa watu wenye ulemavu amekuwa akimzuia mara kwa mara na kuacha lakini wakati mwingine anafanya kinyemela," alisema Ludigija.

Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wafanyabiashara kujiepusha kuruhusu watu ambao hawana mamlaka kwa mujibu wa sheria kufanya kazi ya kuunganisha umeme kwa sababu wanaweza kufanya hivyo kwa kutumia vifaa ambavyo viko chini ya viwango na kutokuwa na utaalamu wa kutosha.

Pia alivipongeza vyombo vya ulinzi na usalama, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano walioutoa wa kufika kwa wakati katika eneo la tukio na kudhibiti moto huo.

Alibainisha kuwa wafanyabiashara hao wenye ulemavu walikuwa na mpango wa kuyaboresha mabanda yao na tayari walishaandaliwa mchoro lakini kabla hawajalikamilisha, tatizo hilo limewakumba.

"Hatupendi moto kwa sababu unarudisha nyuma wafanyabiashara, inaleta machungu. Kwa hiyo tutaendelea kuweka utaratibu kama ambavyo wamefanya soko la Mchikichini juzi. Wameniletea taarifa wameteua kampuni ya ulinzi lakini lazima tuwe na mipango ya uendeshaji wa masoko," alisema Ludigija.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyabiashara Wenye Ulemavu Mkoa wa Dar es Salaam, Juma Hamisi, alisema alipigiwa simu jana saa 11 alifajiri na kujulishwa kuwa soko linawaka moto na kwamba hatua aliyoichukua ni kuwapigia wajumbe wake lakini simu hazikupokewa.

Alisema baada ya hapo, alimtafuta katibu wake na kumpa maelekezo kuwa washirikiane na walinzi kuvunja baadhi ya mabanda ili kuweka uwazi utakaosaidia kuzuia moto kuvuka na kuendelea kusababisha maafa sambamba na kuchunguza wajue chanzo ni nini.

"Baadaye katibu alinijulisha kuwa chanzo ni umeme ulikuwa umekatika. Uliporudi kuna sehemu ya maunganisho pakalipuka na kwa kuwa palikuwa hakuna watu wa haraka, ikasababisha yaliyotokea. Lakini nimekuwa nikimwonya sana anayeunganisha anatambulika kama Mpemba kwamba hana haki ya kuunganisha umeme kwa wafanyabiashara badala yake mwenye mamlaka hiyo ni TANESCO," alisema.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala, Asha Juma, alisema taarifa ya moto waliipata saa 11:40 alifajiri na walijitahidi kufika kwa wakati na baada ya kufika walikuta moto uko katika hatua ya pili na walipambana na hatimaye kufanikiwa kuudhibiti.

# Spika ataka hatua kupaa bei ya bidhaa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameitaka serikali kuchukua hatua kukabiliana na kupanda kwa bei za bidhaa nchini kwa kufuata utaratibu ambao umekuwa ukitumika kunapotokea hali hiyo.

Kiongozi huyo wa Bunge aliagiza hayo bungeni jijini hapa jana, alipokuwa akijibu mwongozo ulioombwa kwake na Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (CCM), aliyetoa hoja ya kutaka chombo hicho kiahirishe shughuli zake za jana ili wabunge wajadili kwa kina kuhusu kupanda kwa bei za bidhaa nchini, ikiwamo vyakula na vifaa vya ujenzi.

Gambo alitumia kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020, inayompa nafasi mbunge yeyote kusimama mara baada ya kipindi cha maswali na majibu na kutoa hoja shughuli za Bunge ziahirishwe ili kujadili jambo la dharura na muhimu kwa umma.

Katika kujenga hoja yake, Gambo alisema kuwa hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza wabunge kuwapa elimu sahihi wananchi wao kuhusu upandaji wa bei za bidhaa muhimu, hivyo akaomba Bunge lipewe nafasi ya kujadili kwa kina jambo hilo.

Alisema wabunge wakijadiliana, itawapa picha nzuri ya nini cha kwenda kusema kwa wananchi wao kuliko ilivyo sasa ambapo bidhaa zinaendelea kupanda, hasa zinazohusu wananchi moja kwa moja.

Akijibu mwongozo huo, Spika Tulia alikiri kuwapo tatizo hilo katika maeneo mengi nchini, akiungana na mbunge huyo kwamba bidhaa zinazowahusu wananchi wa kawaida zimepanda kwa kiasi kikubwa.

Hata hivyo, Spika Tulia alisema hakuridhishwa na hoja ya mbunge huyo kwa namna ilivyo kwa kutumia kanuni ya 54(4) ya kanuni hizo za Bunge ambayo inampa nafasi ya kuagiza kitu gani kifanyike.

"Kutokana na hilo, ninakuagiza Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni (Dk. Dotto Biteko) kwamba jambo hili mlitazame na kufuata utaratibu ambao huwa unatumika katika kusaidia inapotokea bei zinakuwa juu," Spika aliagiza.

Kumeshuhudiwa kupanda kwa kasi kwa bei ya bidhaa mbalimbali nchini hivi karibuni, wabunge wakiitaka serikali kukabiliana na hali hiyo kwa kuchukua hatua madhubuti.


## NOTISI / TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KARIAKOO | UPENDO GODFREY NYANGE | NYUMBA | GODFREY ERASTO NYANGE | BONYOKWA | 27/04/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | KIWANJA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | KIVULE | 27/04/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | SHAMBA | SADIKI NTAHONDI MAPORO | MKURANGA | 22/04/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | LILIAN CLAUDY KANJE | NYUMBA | LILIAN CLAUDY KANJE | MTAA WA MABIBO | 25/04/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | PENDO DANIEL JOHN | NYUMBA | PENDO DANIEL JOHN | KAHAMA -ILEMELA | 28/04/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | MUGANYIZI ERICK EMMANUEL | NYUMBA | MUGANYIZI ERICK EMMANUEL | MBAGALA KUU | 29/04/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | VICTOR MOSES NKO | NYUMBA | VICTOR MOSES NKO | MAJENGO-KIBAIGWA | 27/04/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | TITO KALAM SANGA | NYUMBA | TITO KALAM SANGA | KIBAIGWA | 25/04/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | SEM MOZES DEDE | NYUMBA | SEM MOZES DEDE | IHUMWA-DODOMA | 28/04/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | EDIMUND KAJUNGU MENDRAD | NYUMBA | EDIMUND KAJUNGU MENDRAD | KILOLELI - MWANZA | 25/04/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | LWEYEMAM MEDARD KIBENDERA | KIWANJA | LWEYEMAM MEDARD KIBENDERA | NYASHISHI MWANZA | 25/04/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | NYUMBA | RAJAB MOHAMED MUOMBWA | YANGEYANGE-MSONGOLA | 27/04/2022 NA KUENDELEA |
| AGGREY | MUSTAPHA ABDALLAH ATHUMAN | NYUMBA | MUSTAPHA ABDALLA ATHUMANI | MSONGOLA | 27/04/2022 NA KUENDELEA |
| AGGREY | SALEH ALLY MOHAMED | NYUMBA | SALEH ALLY MOHAMED | MZINGA "B" TUANGOMA | 25/04/2022 NA KUENDELEA |
| AGGREY | GAUDENCIA MATHIAS TEMBA | NYUMBA | GAUDENCIA MATHIAS TEMBA | PUGU STESHENI | 29/04/2022 NA KUENDELEA |
| AGGREY | FREDRICK BALTAZARY PETER | NYUMBA | FREDRICK BALTAZARY PETER | ULONGONI "B" | 29/04/2022 NA KUENDELEA |
| AGGREY | YUSTER WESTON AYOLA | NYUMBA | SHABANI HARUNA MLENDA | MACHINJIONI-MIANZINI | 29/04/2022 NA KUENDELEA |
| AGGREY | JULIAS SIMBO LEMA | NYUMBA | HUSSEIN MTOBA FUNGALINDO | PUGU KINYAMWEZI | 29/04/2022 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0765999000/ 0754497396 / 0652691275/0768672367

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216796702

# TARURA yasitisha utozaji wa faini maegesho magari

**Na Maulid Mmbaga**

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), umesitisha kwa muda usiojulikana utozaji wa faini kwa watumiaji wa maegesho waliopitisha siku 14 bila kulipa madeni ya ushuru wa maegesho kuanzia Machi Mosi, mwaka huu.

Juzi, TARURA ilitoa taarifa ya kuanza kutoza faini kwa watumiaji wa maegesho waliopitisha siku 14 bila kulipa madeni ya ushuru wa maegesho kwa madeni ya kuanzia Machi Mosi na kwamba mchakato huo umesitishwa siku moja baada ya kutangazwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na TARURA, hatua hiyo imekuja baada ya kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali wa maegesho ya kupitia matumizi ya mfumo wa TeRMIS, ambao umeongeza muda wa kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mfumo huo wa kielektroniki.

Sehemu ya taarifa hiyo ilisema: "TARURA inaendelea kuwasisitiza wananchi kuendelea kulipa ushuru wa maegesho kwa wakati ndani ya siku 14 tangu walipotumia maegesho, kama inavyoelezwa katika kanuni za maegesho tangazo Na. 799 la Desemba 3, mwaka jana".

Aidha, ilibainisha kuwa mfumo huo wa malipo ya maegesho kielektroniki TeRMIS unatoa nafasi ya kupata taarifa za kumbukumbu za madeni ya ushuru wa maegesho kupitia simu za mkononi na kwenye programu ya GePG.

# Sweden yaipongeza Tanzania Uhuru wa habari, demokrasia

**Na Richard Makore,** MWANZA

BALOZI wa Sweden nchini, Anders Sjoberg, amesema kwa sasa suala la demokrasia pamoja na uhuru wa vyombo vya habari vimeimarika nchini.

Kutokana na hali hiyo, amewasisitiza waandishi wa habari kuandika habari za uchunguzi ambazo zinalenga kuisaidia jamii.

Alitoa kauli hiyo juzi jijini Mwanza baada ya kusaini makubaliano ya msaada wa Dola za Marekani 500,000 ambazo zimetolewa na nchi yake kwa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za UTPC, Sjoberg alisema suala la demokrasia Tanzania linazidi kuimarika.

Hata hivyo, alisema uwapo wa demokrasia haupimwi kwa kufanyika uchaguzi ulio huru na haki pekee, badala yake inahusisha mambo mengi yakiwamo mashirika ya kiraia kuwa huru na kushiriki.

Alisema demokrasia pia inatakiwa kuhusisha usawa wa wanawake na wanaume pamoja na kuondoa viashiria vya uwapo wa rushwa katika uchaguzi.

Kuhusu uhuru wa vyombo vya habari pamoja na usalama wa waandishi, Sjoberg alisema ni kipaumbele kwa Sweden na kwamba msaada huo utasaidia kuviimarisha vilabu vyao.

"Demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari vinakwenda pamoja na huwezi kuchukua kimoja na kuacha kingine na uhuru wa vyombo vya habari pamoja na usalama wa mwandishi ni kipaumbele cha sera za nje za Sweden," alisema.

Balozi Sjoberg alisema sheria ya kwanza kuhusu vyombo vya habari duniani ilitungwa zaidi ya miaka 250 iliyopita na kuanzia hapo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali.

Sjoberg pia alisisitiza kuwapo kwa waandishi wa habari za uchunguzi ili kujenga uaminifu kwa jamii katika kuleta uwazi na uwajibikaji.

Alisisitiza kwamba msaada huo kwa UTPC utasaidia kukuza uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza pamoja na kuwawezesha waandishi wa habari wa mikoa yote kuandika habari ambazo zitasaidia kukuza uwazi, demokrasia na uwajibikaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Abubakar Karsan, alisema bado wahariri wa vyombo vya habari nchini hawapo huru.

Alisema uamuzi wa mwisho umebaki kuwa wa waajiri pamoja na wamiliki wa vyombo habari, jambo ambalo linarudisha nyuma uhuru wa kuamua ni aina gani ya habari inatakiwa kuchapishwa.

Karsan alisema changamoto nyingine inayovikumba vyombo vya habari ni waandishi wengi kutokuwa na mikataba ya kazi pamoja na kutolipwa mishahara.




Balozi wa Sweden hapa nchini, Anders Sjoberg (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Umoja wa vilabu vya waandishi wa habari Tanzania (UTPC), Abubakar Karsan, wakionyesha nyaraka kwa waandishi wa habari, jijini Mwanza jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya kuendelea kusaidia umoja huo kwa kipindi cha mwaka mmoja. **PICHA: RICHARD MAKORE**

# MOI yapokea wagonjwa 60 uvimbe ubongo

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Mifupa, Upasuji Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), imesema inapokea wagonjwa 50 hadi 60 kwa mwaka ambao wana tatizo la uvimbe kwenye ubongo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respecius Boniface, alitoa takwimu hizo jana hospitalini hapo baada ya wataalam wa MOI kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka India, kufanya upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye ubongo bila kupasua fuvu la kichwa.

Dk. Boniface alitaja sababu za ugonjwa huo ni magonjwa yasiyo ya kuambukiza, watu wenye umri mkubwa na wengine kuzaliwa nao.

"Wagonjwa watatu hadi watano kila mwezi tunawapokea MOI, sijui hospitali nyingine na ambao hawafiki hospitali huko wapo wangapi," alisema Boniface.

Pia alisema hadi sasa MOI imefanikiwa kufanya upasuaji wa kuondoa uvimbe bila kupasua fuvu la kichwa kwa wagonjwa 164 tangu kuanza kwa huduma hiyo Januari mwaka jana.

Alisema mafanikio hayo yametokana na serikali kuwekeza Sh. bilioni 7.9 kwa ajili ya kununua mashine ya kisasa ya matibabu, kujenga miundombinu na kuongeza ujuzi kwa watalaam.

"Wote mmeshuhudia mgonjwa anafanyiwa upasuaji, huku akiwa anaongea na kumaliza bila mgonjwa kupata shida yoyote," alisema. Dk. Boniphace alisema upasuaji huo unatumia njia ya mshipa wa fahamu uliopo kwenye paja kuelekea hadi kwenye ubongo kutoa matibabu hayo.

Alisema pia serikali iliingia ushirikiano na Hospitali ya India kwa ajili ya kuwafundisha watoa huduma za afya wa MOI wanaotoa huduma katika kitengo hicho.

Alisema madaktari hao wameendelea kuja nchini kutoa ujuzi kwa madaktari wazawa kuhusu matibabu hayo ili kuwajengea uwezo na baadaye watoe huduma hiyo wenyewe.

Dk. Boniface alisema tangu wataalam hao wamefika MOI siku tatu wamefanya upasuaji kwa wagonjwa watatu na mgonjwa mmoja anafanyiwa huduma ya upasuaji kwa dakika 30.

Alisema matibabu ya awali mgonjwa alikuwa akifanyiwa huduma ya upasuaji kwa muda wa wiki mbili, lakini kwa sasa mbinu hiyo mpya inatumia dakika 30.

Dk. Boniface alisema gharama za matibabu ya huduma ya upasuaji wa uvimbe kwenye kichwa nje ya nchi inategemea na hali ya mgonjwa lakini kwa wastani ni kati ya Sh. milioni 30 hadi 60, lakini kwa hapa nchini ni Sh. milioni tatu hadi sita.

Alisema pia wataalam wa ndani wataenda nje ya nchi kwenda kujifunza ujuzi wa aina hiyo ili kuongeza idadi kubwa ya wataalam.

Alisema mashine moja ya upasuaji inahitaji watalaam 10 hadi 15 wa kutoa matatibabu lakini sasa wapo 10, na kwamba kwa mwaka mashine hiyo ina uwezo wa kuhudumia wagonjwa 200 hadi 300.

Daktari Bingwa wa Mishipa ya Fahamu na Ubongo, kutoka kitengo cha Upasuaji wa Mishipa ya Ufahamu na Ubongo MOI, Dk. John Mtei, alisema mafunzo hayo yamewasaidia kutoa matibabu mapema kwa wagonjwa wanaofika hospitalini hapo na kupunguza foleni.

# Wajawazito waonywa kujifungulia nyumbani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAJAWAZITO mkoani Shinyanga hasa wa maeneo ya vijijini, wametakiwa kuacha tabia ya kujifungulia nyumbani kwa kuwa maeneo hayo si salama bali waende kwenye huduma za afya ambazo ni salama na kuepuka vifo vitokanavyo na uzazi.

Meneja Miradi kutoka Shirika la Investing in Children and Strengthening their Societies (ICS) mkoani Shinyanga, Sabrina Majikata, alisema hayo juzi wakati akitoa mada ya ajenda ya kitaifa ya malezi inayoitwa 'Familia Bora Taifa Imara, kwa mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani hapa kwenye mafunzo ya malezi bora kwa watoto.

Alisema serikali kwa sasa imeboresha huduma za afya hadi maeneo ya vijijini, hivyo kuwasihi wajawazito waachane na utamaduni wa kizamani wa kujifungulia nyumbani.

"Kujifungua kwenye vituo vya afya kuna faida yake, kwanza mzazi una kuwa salama pamoja na kupewa elimu ya afya ya uzazi kuliko nyumbani ambako ni hatari na unaweza kupoteza maisha,"alisema.

Katika hatua nyingine, aliwashauri wazazi kupanga uzazi wa mpango ili kuzaa wa watoto kwa kuacha nafasi angalau miaka miwili. Alisema hatua hiyo itawezesha kupata muda wa malezi ya mtoto pamoja na kumnyonyesha maziwa ya mama ipasavyo badala ya kushika ujauzito na kumwachisha kunyonya.

Aliwataka pia wanawake pale wanaposhika ujauzito, waanze kuhudhuria kliniki muda wote ili kupata taarifa za maendeleo ya mtoto tumboni hadi wakatapofikia hatua ya kujifungua na kwamba katika kipindi hicho, wajenge tabia ya kula lishe bora na kuacha kufanya kazi nzito.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, walisema jamii bado wana ugumu wa kuendekeza utamaduni wa kizamani licha ya baadhi kuanza kubadilika na kujifungua kwenye vituo vya afya.

Pia waliipongeza serikali kwa kujenga vituo vingi vya Afya na Zahanati katika maeneo mengi hasa vijijini.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (wa pili kushoto), akizungumza na Nahodha Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Abdullah Mwingamno (wa tatu kushoto), wakati wa kupokea meli kubwa aina ya Frontier ACE, iliyobeba magari 4041, iliyotia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya TPA, Ernest Mangu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bandari kavu ruksa kuhifadhi mizigo TPA

**Na Enock Charles**

KUTOKANA na uwapo wa msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, serikali imeagiza kuanzia sasa uhifadhi wa mizigo inayoshushwa katika bandari hiyo uanze kufanyika katika Bandari za Nchi Kavu (ICD).

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam katika hafla ya kupokea meli kubwa ya mizigo iliyokuwa ikiwasili katika Bandari ya Dar es Salaam ikiwa na magari 4,041 kutoka Japan.

Awali, serikali ilipiga marufuku uhifadhi wa mizigo kwenye ICD za watu binafsi mwaka 2015/16, baada ya kuwapo kwa madai ya kujihusisha na ukwepaji kodi.

Katazo hilo lilisababisha mizigo inayoshushwa na meli katika Bandari ya Dar es Salam, husussani magari, kuhifadhiwa kwenye ICD za TPA pekee eneo la bandarini.

Prof Mbarawa alisema vifaa vya kuhifadhia mizigo bandarini vilijaa hadi ukingoni na kusababisha msongamano wa meli, huku meli zikilazimika kusubiri kwa siku nyingi kwa kukosa nafasi ya kushusha mzigo.

"Sasa naagiza magari na makontena yote yaliyopakiwa hapa bandarini yaondolewe na yapelekwe kwenye ICD ili kurahisisha upatikanaji wa nafasi kwa sababu bandari si mahali pa kuhifadhi," alisema.

Prof. Mbarawa alisema serikali imetumia fedha nyingi kupanua Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza idadi ya mizigo. Meli ya mizigo iitwayo MV Frontier Ace kutoka Japan ikiwa imebeba magari 4,041 iliwasili jana ambayo asilimia 73 ya magari hayo yatakwenda nchi jirani.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eric Hamissi, alisema bandari hiyo sasa inatekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuruhusu magari yanayokuja bandarini kukaguliwa kutoka nchi yalipotoka.

Alisema agizo hilo la Rais Samia litarahisisha ufanisi katika bandari hiyo, akisema ukaguzi kutoka nchi yanakotoka ni kiwango cha kimataifa.

Hamissi alisema hadi Februari mwaka huu TPA ilikusanya Sh.bilioni 704 ikilinganishwa na Sh. bilioni 590 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Hivi karibuni, Rais Samia alihoji sababu za magari yanayoingizwa nchini kukaguliwa bandarini, akisema suala hilo husababisha ucheleweshaji usio wa lazima kwa meli.

Rais alimwagiza Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kulifanyia kazi suala hilo kwa kufanya utafiti endapo kuna ulazima wa magari hayo kukaguliwa nchini badala ya nchi yanapotokea.

# Ndoa baina ya wanafunzi yavunjwa kabla kufungwa

**Na Richard Makore,** MWANZA

NDOA ya watoto wawili iliyopangwa kufungwa kati ya mume mwenye umri wa miaka 12 na mke wa miaka 16, imetibuka katika hatua za mwisho katika kijiji cha Getarungu, Serengeti mkoani Mara.

Jeshi la Polisi wilayani humo lilitibua ndoa hiyo huku likiwanasa watu saba, wakiwamo watoto hao ambao ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Kitarungu wilayani Serengeti mkoani Mara.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu juzi, Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Dk. Vincent Mashinji, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo siku tatu zilizopita.

Dk. Mashinji ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Serengeti, alisema ndoa hiyo ilitibuka dakika za mwisho kabla haijafungwa.

Alisema ndoa hiyo ilitarajiwa kufungwa kimila na iliingia doa bada ya vyombo vya dola kuvamia na kuwakamata watu waliohusika nayo.

taarifa zilizokuwa zimetolewa na jeshi la polisi na kuthibitishwa na Dk. Mashinji zilisema watu hao walikamatwa baada ya polisi kupata taarifa za kiintelijensia kwamba watuhumiwa wote, wakiwamo watoto waliotaka kufunga ndoa pamoja na wasimamizi wao, walikamatwa nyumbani kwa bwana harusi.

Watu wanaoshikiliwa katika tukio hilo ni pamoja na Nyang'ombe Magere (50), Ghati Masero (38) ambao ni wazazi wa mtoto wa kiume aliyekuwa anaoa. Wengine ni Kibaki Rioba (23), mkazi wa Sirari wilayani Tarime na watoto wenye umri wa miaka 12 na 16 waliokuwa wanaoana.

Aliyekuwa msimamizi wa ndoa hiyo batili kwa upande wa mwanamume ni mtoto mwenye umri wa miaka 10 (jina limahifadhiwa) na anasoma darasa la pili katika Shule ya Msingi Kitarungu.

Akizungumza kwa sharti la kuhifadhiwa jina lake, mkazi wa Kitarungu ambaye pia ni mwanafunzi wa shule ya msingi, alisema wazazi wa mtoto wa kike walipokea mahari ya ng'ombe sita kutoka upande wa mwanamume ambaye ni mwanafunzi (12) wa darasa la nne.

Mtoa taarifa huyo alisema baada ya wazazi wa mtoto wa kike kupokea mahari, walimkabidhi binti yao kwa mume wake mtarajiwa na maandalizi ya sherehe yakaanza nyumbami kwao mwanamume.

"Baada ya taarifa hizo kufika polisi, askari walivamia sherehe hiyo na kuwakamata watuhumiwa wote na kuondoka nao.

Juliana Kobiro, mdau wa haki za watoto mjini Musoma, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuchukua hatua za haraka kudhibiti uvunjifu wa sheria na haki za watoto.

Alisema hatua hizo zilizochukuliwa zitakuwa fundisho kwa wazazi wanaoozesha watoto wao wakiwa katika umri mdogo badala ya kuwasomesha wapate elimu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunaweza kuepuka Man, Barcelona za Tanzania

**MPIRA** wa miguu ni mchezo maarufu, si Tanzania pekee bali dunia nzima. Umaarufu wa Ligi Kuu ya England (EPL) umevuka mipaka ya nchi hiyo, ambao ni faida kwa klabu kubwa za England.

Klabu kubwa za England zimekuwa zikitumia vizuri wingi huo wa mashabiki hasa katika bara la Asia kwa kufanya ziara za maandalizi ya msimu mpya.

Ukizungumzia mechi za televisheni, ni zile za EPL ndizo zinazoongoza nchini kwa mashabiki kufurika katika maeneo mbalimbali kila mechi zinapochezwa, tena nyingine hushuhudiwa usiku mkubwa.

Ziara hizo mbali ya kuwa sehemu ya maandalizi ya timu lakini pia hutumika kwa kuuza vifaa mbalimbali vya timu kama jezi.

Kutengeneza wigo wa washabiki si kitu kidogo wala cha mzaha. Ukifuatilia historia ya klabu nyingine za England na sehemu nyingine duniani utabaini kuwa zimetumia muda mrefu kutengeneza washabiki kutokana na ukweli kuwa kuna klabu nyingi huko kwao.

Nyingi ya klabu hizo zimeasisiwa karibu au zaidi ya karne moja iliyopita, na sasa zimekuwa taasisi kubwa, tena si tu katika kucheza mpira wa miguu, bali heshima ambayo zimejijengea.

Hapa Tanzania tuna klabu kongwe na zenye wafuasi wengi za Simba na Yanga. Klabu hizi za Dar es Salaam zimeanzishwa zaidi ya miaka 80 iliyopita. Kimsingi klabu hizi ni za aina yake, kwani zina hazina ya washabiki.

Wakati klabu nyingine zinafikiria na kujipanga kwa ajili ya kutengeneza wigo wa mashabiki, zenyewe zina wafuasi wa kutosha. Wafuasi ni zaidi ya mashabiki, kwani hao wameshaamini katika Yanga na Simba. Huwezi kuwabadili kutoka kushabikia timu hizo.

Hawa iwe ni wafuasi, mashabiki au wanachama tu wao hawazitazami klabu zao katika mwelekeo mwingine zaidi ya ushindi. Kwao maendeleo katika klabu ni ushindi tu, iwe kiwango cha mchezo unaochezwa ni mbovu lakini kinatoa matokeo wao hilo si tatizo.

Ni historia kwa sababu sasa hivi ukikutana na mfuasi wa Yanga au Simba mwenye umri wa miaka 50 hawezi kukupa sababu yenye mantiki ni kwa nini alifikia kuipenda klabu anayoishabikia.

Lakini leo ukifuatilia kwa karibu utabaini kuwa si mashabiki tu, bali Tanzania kuna timu zinaitwa Manchester United, Arsenal, Liverpool, Barcelona, West Ham, Real Madrid, Real Zaragoza, AC Milan, Inter Milan, Panama na nyingine, na zinacheza ligi zetu.

Kimsingi ili timu iweze kucheza ligi yoyote rasmi- ile inayotambuliwa na chama cha mpira wa miguu cha wilaya, chama cha mpira wa miguu cha mkoa au Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ni lazima iwe imesajiliwa.


Ni vizuri wasajili wetu na hata waanzilishi wa Manchester United ya Tanzania wakafahamu kwa nini hiyo ya England imeitwa Manchester United, ile ya Hispania inaitwa Barcelona au ile ya Italia inaitwa AC Milan.

Sisi Nipashe tunaona kwamba, jambo la kwanza ambalo tunatakiwa kufahamu ni kuwa majina kama Manchester, Barcelona, Madrid, Milan, Tottenham, Blackburn ni miji au vitongoji katika nchi hizo za Uingereza, Hispania na Italia.

Hivyo, klabu hizo mara tu zilipoanzishwa zilianza kuwa na washabiki katika maeneo yao kwa sababu majina tu yanawakilisha miji husika. Mbeya City au Musoma Shooting zina uhalali wa kujitengenezea washabiki katika miji hiyo kwa sababu hiyo niliyoitaja hapo juu.

Tunaona kwamba, sasa ni wakati kwa Ofisi ya Msajili wa Klabu na Vyama vya Michezo nchini wakati wa kusajili klabu kuangalia zaidi ya malengo na madhumuni katika katiba za klabu zinazoomba kusajiliwa. Maana ya majina ya klabu husika nayo iangaliwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Morrison akitumiwa, Simba itavuna mabao

**KWENYE** mechi mbili za hivi karibuni ambazo Simba imecheza dhidi ya US Gendarmerie ambayo ilikuwa ni ya Kombe la Shirikisho, pamoja na ile ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union imeonyesha kuwa timu hiyo inatengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini kwa bahati mbaya hazitumiwi vizuri.

Licha ya kushinda mabao 4-0 kwenye mechi hiyo ya mwisho wa makundi, wachezaji wa Simba walitengeneza nafasi nyingi hasa kipindi cha kwanza, lakini walishindwa kuuweka mpira wavuni.

Hiyo iliwaweka juu wanachama na mashabiki wa timu hiyo, mpaka pale walipojirekebisha kipindi cha pili na kufanikiwa kupata mabao na kwenda kwenye hatua ya robo fainali.

Kwenye mechi dhidi ya Coastal Union hali iliendelea kuwa vile vile. Ilitengeneza nafasi nyingi za kufunga, hasa kipindi cha pili wapinzani waliposawazisha, lakini wachezaji wa timu hiyo walionekana kuwa na matatizo wanapofika karibu na lango, mpaka pale Meddie Kagere alipoweka bao la pili dakika za majeruhi.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola akakiri kuwa wamekuwa na udhaifu huo wa kukosa mabao mengi ya wazi.

"Suala hili tumekuwa tukilifanyia kazi sana kwenye uwanja wa mazoezi. Lakini tutaendelea kurekebisha ili kupata mabao mengi kwenye mechi, kwa sababu tunatengeneza nafasi nyingi, ila kuzitumia tu ndiyo tatizo," alisema Matola.

Ukiingalia Simba ni moja kati ya timu inayotengeneza nafasi nyingi si kwenye mechi hizi mbili tu, bali tangu msimu huu umeanza.

Ila kwa bahati mbaya mastraika wake wameshuka viwango vya kutumbukiza mpira ndani ya wavu.

Kinachotakiwa kwa sasa ni kusaidiwa tu kuweza kupata nafasi rahisi za kufungwa na si vinginevyo.

Simba ambao ndiyo wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, inakwenda kucheza dhidi ya Orlando Pirates kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), Aprili 17, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Marudio ya mechi hiyo watachezwa Aprili 24, nchini Afrika Kusini. Ni mechi ya mtoano ambayo Simba inaanzia nyumbani, hivyo inatakiwa imelize mechi hiyo mapema.

Nina maana inatakiwa ifunge mabao mengi iwezekanavyo. Lakini hayafungwi kwa domo, bali ni lazima vitu vifanyike.

Pamoja na yote, kufunga ni sanaa. Si kila mtu anajua kufunga. Kwa maana hiyo benchi la ufundi la Simba lingetafuta namna ya kufanya ili wapate mabao mengi.

Niliona kwenye mechi didi ya US Gendarmarie, kulikuwa na namna fulani ya uchoyo kwa baadhi ya wachezaji wa Simba, ambao kila mmoja akifika golini anataka kupiga tu ili afunge. Hakuna bao linalofungwa namna hiyo.

Mpira ni mchezo wa ushirikiano, haiwezekani mchezaji yupo pembeni kidogo mwa lango anataka kulazimisha kufunga badala ya kumpa mchezaji mwenzake.

Bernard Morrison, ndiye aliyeongoza kwa kuingia ndani ya boksi na kukosa mabao. Hata kwenye mechi dhidi ya Coastal ni hivyo hivyo. Matola anasema analifanyia kazi suala hilo yeye na kocha wake mkuu, Pablo Franco.

Mimi nitoe ushauri tu kuwa kama watamtumia Morrison vizuri, Simba inaweza kupata mabao kuanzia matatu hadi matano kwenye mechi ya kwanza.

Kwanza kabisa ni lazima aanze, kwa sababu ni mchezaji mwenye uthubutu, ambaye akipata mpira anachojua ni kulitafuta eneo la wapinzani na si kuangalia, au kurudisha mpira nyuma.

Atengenezwe kuwa mpishi wa mabao kwa wenzake, ambao naona wanaweza kufunga mabao rahisi sana na mengi.

Akipata mpira huwa mtata, kwa kupiga chenga za maudhi na kuingia ndani ya hatari, lakini tatizo hutaka kufunga mwenyewe, huku wenzake wakiwa wanamtazama tu.

Pamoja na uwezo wake huo mkubwa, Morrison hata sanaa na kufunga mabao. Angekuwa anatengenezwa kupiga krosi na kutoa pasi za mwisho kila anapopata mpira, basi Simba ingevuna mabao mengi sana.

Kwenye mechi dhidi ya Orlando Pirates, benchi la ufundi la Simba linatakiwa kumuambia kuwa yeye asiwe mfungaji kwenye mechi hiyo, bali ni mtoa pasi za mwisho tu na si vinginevyo.

Akipewa kazi hiyo, kwa sababu anafuatwa na mabeki wengi, inaweza kuwa nafuu na mastraika wa Simba na wengine wakijazana golini kuweka mipira ndani ya wavu. Morrison si muoga wa kulitafuta boksi, hivyo anatakiwa awe anawavuta, na yeye akatoa pasi ambazo zitawakuta wenzake wako kwenye eneo sahihi kwenye mapana ya goli na kufunga mabao rahisi.

Hii itawafanya kupata mabao mengi, ambayo yatawaweka salama kuelekea kwenye mechi ya marudiano Sauzi.

## Serikali yaonya askari mgambo

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema mgambo hawatakiwi kuhusika katika kuwapanga wala kuleta bugudha yeyote kwa wafanyabiashara wadogo(machinga) nchini.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo.

Katika swali lake, Gambo alihoji sababu za machinga kutopata vitambulisho vya ujasiriamali na wanaendelea kutozwa ushuru na Halmashauri ya Jiji la Arusha.

"Mgambo wa Arusha wamekuwa wakipora vitu vya watu na kuweka kule 'depot' vinaoza na wanachukua fedha za watu nje ya utaratibu na manyanyaso," alisema.

Dk. Dugange alisema serikali ilishatoa tamko kuwa katika shughuli za kuwapanga machinga nchini mgambo hawahusiki na hawatakiwi kuwabugudhi wafanyabiashara.

"Niwaombe Jiji la Arusha kusimamia maelekezo ya serikali wafanyabishara wasibugudhiwe na mgambo sehemu yeyote," alisema. Dugange pia alisema suala la baadhi kutopata vitambulisho ni suala la kutoa elimu kuhamasisha kwa hiari yao wapate vitambulisho.

Alisema Halmashauri inaendelea kuwaelimisha wafanyabiashara waliobaki wawe na vitambulisho.

Katika swali lake la msingi, Gambo alihoji Halmashauri ya Jiji la Arusha ina machinga wangapi na wako maeneo gani na idadi gani wameshapatiwa vitambulisho hadi mwishoni mwa Februari, mwaka huu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Dugange alisema hadi kufikia Februari, Jiji la Arusha lilikuwa na machinga 5,426 ambao walikuwa wamepangwa katika maeneo mbalimbali.

Alitaja maeneo hayo ni soko la Samunge, Kiwanja Soko la Kilombero, Eneo la Ulezi Mianzini, Machame Luxuaryna Kilombero Eneo la Daladala.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea kuratibu usajili na utoaji vitambulisho vya machinga na kwa halmashauri hiyo, machinga 1,187 sawa na asilimia 22 wamekwishapatiwa vitambulisho.

# Mbunge ataka jeshi jamii ulinzi watoto

MBUNGE wa Viti Maalum, Nusrat Hanje, ameishauri serikali kuanzisha Jeshi Jamii kwa ajili ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia na utumikishwaji watoto.

Alitoa ushauri huo wakati akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana na kuhoji kama serikali haioni umuhimu wa kuwa na jeshi la aina hiyo,

"Kwa nini wakati huu serikali isiwe na jeshi jamii kama ilivyo jeshi usu kwa upande wa maliasili ili kuhakikisha jamii inalinda watoto wetu dhidi ya ukatili?" alihoji huku akisisitiza kwa nini serikali isianzishe klabu za stadi za maisha kwenye shule ili kuwajengea uwezo watoto kujilinda.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, alisema wizara imejipanga kupitia Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ili kuhakikisha wanakuwa na usalama kuanzia ngazi za vijiji hadi mkoa na unahusisha vyombo vya ulinzi na usalama.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kuzuia ukatili wa kijinsia na utumikishwaji wa watoto katika kambi zinazotarajiwa kujengwa ili kuwezesha ujenzi wa Bomba la Mafuta Hoima Tanga.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema katika kuhakikisha vitendo vya ukatili wa kijinsia na utumikishwaji wa watoto vinakomeshwa katika maeneo mbalimbali nchini, ukiwamo Mradi wa Bomba la Mafuta.

Kupitia MTAKUWWA), alisema wizara imejipanga kuimarisha na kuzijengea uwezo kamati za ulinzi na usalama kwa watoto.

Pia alisema serikali itaendelea kutumia vyombo vya dola kuhakikisha wale wote wanaotumikisha watoto na kufanya vitendo vya ukatili wanachukuliwa hatua za kisheria.



Mbunge wa Msalala, Kasimu Idd, akiuliza swali la nyongeza kwenye vikao vya Bunge la bajeti vinavyoendelea, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoso la sensa lazingatia ulemavu

BUNGE limeelezwa kuwa dodoso la Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika nchini Agosti, mwaka huu, limejumuisha maswali 10 yanayohusu hali ya ulemavu.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Khadija Taya.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 inajumuisha kupata takwimu sahihi za watu wenye ulemavu na aina ya ulemavu wao.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chande, alisema maswali hayo yataulizwa kwa watu wote ikijumuisha umri, jinsi na ulemavu na hivyo kutoa takwimu za hali ya ulemavu nchini.

"Kupitia sensa hiyo, ni matarajio yetu kuwa Serikali itapata takwimu rasmi za hali ya ulemavu nchini kwa maeneo ya kiutawala, jinsi, hali ya ndoa, kiwango cha elimu, ajira na viashiria vingine muhimu vilivyoainishwa katika dodoso la Sensa,"alisema.

Alitoa wito kwa Wabunge kuungana na Serikali kuwahimiza wananchi kushiriki kikamilifu katika Sensa ya Watu na Makazi itakayofannyika Agosti 2022.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali imejipangaje kupitia Wizara hiyo kuondoa kero za watu wenye ulemavu.

Akijibu swali hilo, Chande alisema baada ya kukamilisha sensa na kupata takwimu sahihi za watu wenye ulemavu ili kusaidia kuandaa mipango na kutoa vipaumbele ambavyo vitaingizwa kwenye bajeti.

"Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan haipo tayari kumuacha mtu nyuma na watajumuishwa kwenye vipaumbele vya nchi hii kwa maslahi ya umma,"alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**



Mwezeshaji kutoka Taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Hans Obote, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbagala Kuu, wakati wa kampeni ya kupinga rushwa ya ngono kwa wanafunzi iitwayo 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', inayoendeshwa na taasisi hiyo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wapewa somo viashiria rushwa ya ngono

**Na Sabato Kasika**

WANAFUNZI wametakiwa kuwa makini kwa kutambua viashiria vya rushwa ya ngono vinavyotumika kuwanasa na kuviepuka ili kutimiza ndoto walizojiwekea kwenye elimu.

Mwezeshaji wa Taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Hans Obote, alisema hayo juzi alipokuwa akitoa elimu ya kupinga rushwa ya ngono kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani Dar es Salaam.

Mwezeshaji huyo alikuwa katika mwendelezo wa kampeni za taasisi hiyo iitwayo 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', ambazo zinalenga kukomesha rushwa na ukatili wa kijinsia.

Miongoni mwa shule hizo ni Mbagala High School na Mbagala Kuu Sekondari ambapo aliwataka wanafunzi kuwa makini dhidi ya rushwa hiyo kuanzia nyumbani, mitaani na hata hata shuleni.

Alitaja shule zingine zilizofikiwa katika mwendelezo wa kampeni hiyo inayofadhiliwa na Women Fund Tanzania (WFT) ni shule za msingi Mchikichini, Gongo la Mboto JICA, Mwangaza na Maarifa huku akiwakumbusha madhara ya rushwa. "Tambueni kuwa kupewa zawadi ndogo ndogo bila kuombwa, lifti zikiwamo ya bodaboda ni miongoni mwa viashiria na mbinu zinazotumiwa na mafataki kwa lengo la kuwanasa kirahisi, zikakataeni," alisema.

Obote alisema rushwa hiyo ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya elimu na kwamba imesababisha wengi wao kutofikia malengo, ambapo amewataka watambue viashiria hivyo na kuvikwepa.

"Miongoni mwa viashiria hivyo ni mtu kumpa zawadi ndogo ndogo mwanafunzi bila kuombwa, kumpa lifti ikiwamo ya bodaboda kama njia ya kumvutia ili iwe rahisi kumnasa, hivyo kuweni makini na hayo," alisema Obote.

Mwezeshaji huyo alisema wanafunzi na wanawake kwa ujumla, wamekuwa wakiathirika kwa kiasi kikubwa kwa rushwa hiyo hasa wanapotoka nyumbani na kwenda shuleni au kazini.

Alisema kutokana na mazingira hayo, WAJIKI imekuwa ikipambana na rushwa hiyo kupitia kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' kwa kutembelea shule mbalimbali na kuelimisha wanafunzi.

"Lakini pia katika jamii, huwa tunaitisha mikutano kwa kushirikisha wadau wetu wakiwamo polisi, TAKUKURU, maofisa wa maendeleo ya jamii, madereva wa bodaboda, bajaj na daladala na kutoa elimu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI, Janeth Mawinza, alisema taasisi yake inashirikisha wadau mbalimbali kwa lengo la kupata njia bora ya kumlinda mtoto wa kike dhidi ya rushwa ya ngono.

"Suala la mapambano dhidi ya rushwa ya ngono na ukombozi wa mwanamke ni jukumu la kila mmoja na kila kundi liliongelee ili liweze kutokomezwa na kuleta mapinduzi katika vita hiyo," alisema Mawinza.

# Fikra mgando kikwazo vijana 'kutoboa'

**Na Francis Godwin,** IRINGA

SABABU kubwa ya baadhi ya vijana kutoka familia zenye mazingira magumu kutokuanzisha miradi ya kiuchumi ni kutokana na kujinyanyapaa na kukata tamaa kuwa hawawezi kufanikiwa kiuchumi hata kama watawezeshwa, imeelezwa.

Akizungumza jana katika ukumbi wa Yatima, Kijiji cha Igoda, Mufindi mkoani Iringa mara baada ya mafunzo ya mtazamo na miradi ya kilimo na ufugaji, Meneja Msaidizi wa Mradi wa Vijana, Danford Mkumba, alisema changamoto ya vijana wengi ni kutawaliwa na fikra mgando katika maisha na hiyo ndiyo sababu ya kutokufanikiwa.

Mkumba alisema hayo katika mafunzo yanayotolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ya R - LABS Tanzania kwa vijana wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM).

Alisema vijana wanayo fursa kubwa ya kufanikiwa katika maisha kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na YAM pamoja na serikali kupitia halmashauri zote nchini ambazo zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya mikopo isiyo na riba kwa vijana ,wanawake na watu wenye ulemavu .

Meneja huyo alisema mafunzo hayo yamelenga kuwafundisha vijana kujitambua kifikra na kuondokana na fikra mgando ili kusonga mbele kimaisha kwa kuibua miradi ya kiuchumi kupitia rasilimali zinazowazunguka.

Mkumba alisema baadhi ya vijana wanaamini kuwa wakitoka katika familia duni kwao ni vigumu kufanikiwa katika maisha lakini kutokana na mafunzo hayo, vijana watajitoa katika fikra mgando na kwenda na fikra inayokua.

Washiriki wa mafunzo hayo Diana Yohana, Saraphina Tengelakwi na Anderson Mpende, walisema kutokana na mafunzo waliyopewa, wana matumaini makubwa ya kubadili maisha kwa kubuni na kuendesha miradi ya kiuchumi.

Diana alisema kutokana na ulemavu wake wa ngozi, jamii inayomzunguka imekuwa ikitoa upendeleo mkubwa kwake na shida ya kutokuwa na mradi wa kufanya ni kutokana na kupata mimba za utotoni hali iliyosababisha kukwamisha ndoto yake ya kusonga mbele kimaisha hasa katika masomo .

Alisema kwa mafunzo hayo ya kuondokana na fikra mgando iliyokuwa imemtawala, anaamini atakuwa mfano mwema kwa kuanzisha mradi wake au kutimiza ndoto yake ya kurudi shuleni kwenda kusomea ualimu ili kuja kufundisha wenzake .

Saraphina alisema sababu kubwa ya vijana kutokuwa na miradi ni kutokana na uwezo wao wa kufikiri kimaendeleo na wengi wao kuishia kufikiri kurudi nyuma kwa kutazama familia wanazotoka zilivyo duni na kukatishwa tamaa ya kusimamia kufanya shughuli za kiuchumi.

Mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) umelenga kuwawezesha zaidi ya vijana 770 wakiwamo watoto 150 yatima kutoka kata hizo tatu ambazo zote zitaunganishwa na vijiji 16 za mradi huo.

Aidha, mradi huo ni wa miaka minne tangu mwaka 2021 hadi 2024 na umefadhiliwa na serikali ya Finland chini ya taasisi yake ya Diaconess kwa ushirikiano wa serikali ya Tanzania chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na taasisi ya Foxes Community and Wildlife Conservation.

# Wakulima pamba wapata mkombozi

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kuongeza thamani ya zao la Pamba nchini, Kampuni ya MO Green inayohusika na uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo, imezindua aina mpya ya kiuatilifu cha Mo Strong kinachoua wadudu wanaofyonza na kukata pamba.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Matolo Felician, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema kiuatilifu hicho kina uwezo wa kumsaidia mkulima kuzalisha pamba bila kupata uharibifu kwa asilimia 100.

Alisema kiuatilifu hicho kimefanyiwa majaribio katika zao hilo na kimefanya vizuri na wakulima wameridhishwa na utendaji kazi wake.

"Serikali inaamini kwenye kilimo na kukuza uchumi na kiuhalisia sisi MO Green tunaushahidi huo wa kupanda kwa uchumi kwa kuangalia baadhi ya nchi ambazo uchumi wake umekuwa chanzo kikuu ni kilimo," alisema Felician.

Alisema kampuni hiyo inajikwamua kiuchumi kutokana na ubora wake na bei nafuu na kwamba wanaendelea kumsaidia mkulima kwa kumuuzia bidhaa hiyo kwa Sh. 8,000 hadi 10,000 ambayo itatosha kupuliziwa kwenye shamba la ukubwa wa ekari moja.

Kiuatilifu hicho, kwa mujibu wa Felician, kina uwezo wa kupambana na wadudu aina ya kangambili na chawa wa jani ambao wote wanaharibu pamba.

Alisema kiuatilifu hicho kinachozalishwa nchini China, tayari kimsambazwa kwenye maduka ya pembejeo kote nchini na ofisi za bodi ya pamba.

Naye Ofisa Kilimo wa kampuni hiyo, Alex Michael, alisema mbali na kiuatilifu hicho, pia wanatoa huduma za mbolea ambazo zina ubora unaokubalika.

Alisema kiuatilifu hicho kina uwezo mkubwa wa kuua wadudu waharibufu wa pamba kwa njia ya mguso.



## Wang'atwa sikio kuhusu mazingira

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Jiji la Dodoma wametakiwa kulinda na kusimamia miundombinu ya uboreshaji wa mazingira inayowekwa katika barabara mbalimbali.

Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, alisema hayo jana alipokuwa akikagua miti ya maua iliyowekwa kwa ajili ya kulipendezesha jiji katika barabara mbalimbali.

Kimaro aliwakumbusha wakazi wa Dodoma kuwa mabalozi wa kulinda na kuisimamia miti ya maua iliyowekwa barabarani ili isiharibiwe.

"Baadhi ya maeneo ya barabara ambayo yamepandwa miti ya maua kwenye vyungu, tayari vimeharibiwa na vingine kutumiwa kama sehemu ya kuwekea uchafu tabia hii inatakiwa kukemewa na kila mtu.

"Hapa niwaambie wakazi wa Dodoma kuwa kwa yoyote atakayebainika kuhujumu, kuharibu miti hiyo ya maua iliyowekwa barabarani, Jiji litalazimika kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kuwatoza faini kuanzia 50,000 hadi 300,000," alisisitiza Kimaro.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akiwaongoza wadau wa mazingira wa jiji hilo kupanda miti ya maua kwa ajili ya kuzipendezesha barabara, aliwataka wadau wa mazingira ambao majengo ya ofisi yako barabarani, kuilinda na kuisimamia ili isiharibiwe.

"Miti hii ya maua tumeipanda kwenye vyungu vinatakiwa kusimamiwa na kulindwa na wale wote ambao majengo na maeneo yao ya kufanyia kazi yako jirani na miti hiyo wahakikishe wanailinda kwa uaminifu mkubwa," alisema Shekimweri.

# Bahi yamwagiwa mil. 230/- kukabili utoro wanafunzi

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WILAYA ya Bahi mkoani Dodoma imezindua mradi wa kukabiliana na wanafunzi kukatisha masomo katika shule nane za msingi na sekondari utakaogharimu Sh. milioni 230 na zaidi ya wanafunzi 3,600 watanufaika.

Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Wilaya ya Bahi, Boniface Wilson, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa mradi huo.

Alisema Bahi ni kati ya wilaya 20, zilizoandika andiko la kupata fedha kutoka Shirika la Misaada la Korea Kusini (KOICA), ambalo lilifanya utafiti katika halmashauri 20 zinazokabiliwa na tatizo la wanafunzi kutokumaliza masomo kwa kiasi kikubwa.

"Mradi huu umezinduliwa rasmi leo (jana) na Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mnkunda, na sisi Bahi ni kati ya wilaya tano nchini ambazo zimepata fedha za kutekeleza mradi huu kati ya halmashauri 20 zilizoandika maandiko yao," alisema.

Alisema kiasi hicho cha fedha ni kwa ajili ya mwaka mmoja na kama watafanya vizuri mradi utaendelea kupata fedha katika miaka inayofuata.

"Shughuli zinazofanyika katika mradi huu ni pamoja na kuelimisha wananchi umuhimu wa elimu ili watoto kumaliza elimu yao ya msingi na sekondari," alisema.

Wilson alisema mradi huo pia unawezesha wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu kwa kuwanunulia vifaa vya shule vikiwamo sare, madaftari na viatu.

"Lakini wanafunzi wengi hawaji shuleni kutoka na ukosefu wa chakula, hivyo tumeandaa mpango wa kutoa uji kwa wanafunzi wote katika shule nane, za msingi tatu na sekondari tano ili kukomesha mdondoko wa wanafunzi," alisema.

Pia alisema maradi huo unajihusisha na utoaji wa elimu kwa viongozi wa vijiji kuelekezwa namna ya kuzuia wanafunzi kuacha masomo ili wote wanaoanza darasa la kwanza wamalize darasa la saba na kidato cha kwanza wafike cha nne.

"Pia tunafundisha walimu mbinu za kuvutia watoto wapende shule kwa kutoa sare za shule na mahitaji mengine ya muhimu lakini pia uji kwa wanafunzi wote na michezo inatumika kuwavuta watoto kuja shuleni," alisema.

Kadhalika alisema mpango huo utasaidia kuongeza mahudhurio na ufaulu kwa wanafunzi kutokana na idadi kubwa kushiriki ratiba za masomo kikamilifu tofauti na hapo awali.

"Mpango huu kabla ya mkuu wa wilaya kuuzindua leo, kuna baadhi ya shughuli zilishaanza ambazo kwa kiasi kikubwa zimesadia hata matokeo ya mtihani ya Moko, Shule ya Msingi Uhelela kupanda tofauti na ilivyo kuwa hapo zamani," alisema.

Mwakilishi wa Kampuni ya Kibaigwa Flour, Kelvin Msola, ambayo imepewa zabuni ya kusambaza unga wa uji kwa ajili ya shule hizo, alisema mpango huo utasaidia kupunguza tatizo la utapiamlo kwa watoto.

"Unga ambao tunausambaza katika shule hizi unavirutubisho vingi umechanganywa na maziwa,soya,mahindi,sukari na una zaidi ya vitamini 16 na madini kwa ajili ya kujenga afya ya ukuajia wa motto," alisema.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akisalimiana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Vodacom Group, Shameel Joosub, wakati wa uzinduzi wa mfumo wa Vodacom m-mama, jijini Dodoma mapema wiki hii, utakaosaidia kuwapa usafiri kinamama wajawazito na watoto wachanga pindi wanapopata dharura. Katikati ni Ofisa Mkuu wa Biashara Kimataifa wa Vodacom Group, Diego Gutierrez. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoa mapendekezo kuiboresha demokrasia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAJUMBE wa mkutano wa kitaifa wa maridhiano, haki na amani wametoa mapendekezo 15 yatakayowezesha kufanyika kwa marekebisho ya sheria ya uchaguzi na ile ya vyama vya siasa ikiwamo matokeo ya urais kuhojiwa mahakamani na kuwepo kwa mgombea binafsi.

Mkutano huo uliandaliwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), uliofanyika jijini Dodoma kwa siku mbili ukihusisha wadau mbalimbali wa masuala ya siasa na demokrasi ndani na nje ya nchi ambapo ufunguzi wake ulifanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Akisoma mapendekezo hayo kwa niaba ya wajumbe wa mkutano huo, Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu, alisema mapendekezo hayo kabla ya kumfikia Rais, yatafikishwa kwanza kwa mwenyekiti wa kikosi kazi cha kukusanya maoni.

Semu alisema mapendekezo mengine ambayo wajumbe wameyatoa kwa ajili ya kufanya marekebisho ya sheria ya uchaguzi ni Rais ashinde nafasi kwa kupata asilimia 50 ya kura jumlisha moja.

"Maazimio kuhusu uchaguzi huru na wa haki, matokeo ya urais yahojiwe mahakamni kuwepo na mgombea huru na kusiwapo na mgombea ambaye atapita bila kupingwa na kama ikitokea hivyo, basi apigiwe kura ya ndiyo au hapana," alisema.

Pia alisema wajumbe wamependekeza mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi Zanzibar kwa kutaka kuondolewa kwa utaratibu wa kutumia masheha katika kuandikisha wapigakura katika daftari la kudumu la wapigakura.

"Pia wajumbe tumekubaliana kutokuwapo kwa matumizi ya nguvu za dola siku ya uchaguzi na kuondoa kura ya mapema na tume za uchaguzi zifuate sheria na maadili katika kusimamia uchaguzi mkuu," alisema.

Vilevile, alisema wajumbe wametoa mapendezo kuhusu ustawi wa demokrasia ya vyama vingi na kusisitiza kuwa ruzuku zitolewe kwa vyama vyote vya siasa.

Kadhalika, alisema wamekubaliana uwapo ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika ngazi za uamuzi ndani ya vyama vya siasa ikiwamo kuheshimu katiba na sharia na kuruhusu mikutano ya vyama vya siasa.

"Maazimio kuhusu majadiliano kwa lengo la kuleta maridhiano haki na amani, wadau wote kukiri pale tulipokosea ili kuleta maridhiano ya kweli hususani tume za uchaguzi chama tawala serikali na wadau wengine," alisema.

Alisema maridhiano yasimamiwe kwa kutungiwa sheria na kurekebisha katiba pale inapobidi.

"Mkutano kama huu ufanyike na Zanzibar na kuangalia changamoto zinazotokea kwa upande huo wa Muungano, kufanyia kazi kwa haraka changamoto za Tanzania Bara ili yaliyojitokeza upande wa Zanzibar yasitoke Tanzania Bara," alisema.

Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, akimwakilisha Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliwapongeza wajumbe wa mkutano huo kwa mapendekezo hayo na kuahidi kuwa serikali itayafanyia kazi.





# Waziri aeleza namna ya kumuenzi Karume

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

VIJANA wametakiwa kumuenzi kwa vitendo aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, kwa kuisoma historia ya nchi ili kujua walikotoka kwa lengo la kuvirithisha vizazi vijavyo historia hiyo.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, alisema hayo jana wakati akifunga maonyesho maalum ya Karume katika Mnara wa Kumbukumbu ya Mapinduzi, Kisonge mjini Unguja.

Alisema kuna haja ya vijana kusomeshwa historia ya Karume wakiwa shuleni ili historia hiyo igande vyema katika vichwa vyao.

Waziri Rahma alisema katika zama hizi za mitandao ya kijamii, vijana pia wanatakiwa kujitahidi kuchambua historia sahihi ya Karume ili kuepuka kupotoshwa na watu wabaya.

Pia aliwashauri wataalam wanaoijua vyema historia ya kiongozi huyo, waitumie mitandao ya kijamii kuiingiza historia yake katika mitandao hiyo.

Akielezea lengo la maonyesho hayo, Waziri Rahma alisema ni kumuenzi mwasisi huyo aliyepigania uhuru wa Zanzibar ili wananchi kujikomboa kutoka kwenye ukoloni.

Msimamizi Mkuu wa Makumbusho ya Miaka 50 ya Mapinduzi Mnara wa Kumbukumbu Kisonge, Ali Ussi Khamis, aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi katika makumbusho hayo ili kujifunza mengi ambayo hawayajui kuhusu nchi yao.

Pia aliwataka wananchi kuyaendeleza mazuri yote yaliyofanywa na Mzee Karume kwa lengo la kuiletea maendeleo Zanzibar.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar (KIST), Dk. Mahmoud Abdulwahab Alawi (kulia), akikabidhiana hati ya makubaliano ya pamoja na Tom Peeter kutoka Chuo cha AP Hogeschool Antwerpen cha nchini Belgium, kwaajili ya kukuza na kubadilishana uzoefu katika hafla iliyofanyika Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mazrui ataka kazi mapambano malaria

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wafanyakazi wa Kitengo cha Malaria kuongeza bidii kuwahamasisha wananchi kutumia vyandarua vilivyotiwa dawa ili kumaliza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2023.

Alisema hayo jana katika ziara ya kuzitembelea taasisi za wizara zikiwemo kitengo cha kupambana na kumaliza malaria, Kitengo Shirikishi cha Afya ya Uzazi na Mtoto na Kitengo cha Afya ya Akili.

Waziri Mazrui alisema lengo la kufanya ziara hiyo ni kujua maendeleo na changamoto wanazokabiliana nazo wafanyakazi wa taasisi hizo ili kuzitatua na kuleta ufanisi katika kazi zao.

Meneja Programu Kitengo cha Kupambana na Malaria, Moh'd Ali, alieleza baadhi ya changamoto zinazowakabili ni pamoja na ongezeko la wagonjwa wa malaria asilimia 68 kutoka nje ya Zanzibar, maambukizi kwa wanafunzi wa bweni wa muda mfupi na uchakavu wa jengo.

Aliiomba Serikali kusaidia upatikanaji wa vyandarua sambamba na kampeni ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali hasa sehemu zinazotuwama maji.

Naye Kaimu Meneja Kitengo Shirikishi cha Afya ya Uzazi na Mtoto, Farhat Khalid, alizitaja changamoto wanazokabiliana nazo katika kitengo hicho kyuwa ni vifo vya watoto, kupungua kwa asilimia ya watoto wanaopelekwa kupatiwa chanjo katika baadhi ya wilaya na upungufu wa fedha za uendeshaji wa ofisi.

Hata hivyo, Waziri Mazrui aliwataka maofisa na watendaji wa vitengo hivyo kushauri namna bora ya kuondokana na changamoto hizo ili lengo la kuimarisha afya za wananchi wote litimie.

# Asisitiza matumizi TEHAMA kwa elimu

Na Mwandishi Wetu

MKURUGENZI Mtendaji Vyuo vya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Ali Silima, amesema matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni njia pekee ya kurahisisha shughuli za elimu katika maisha ya hivi sasa.

Alisema hayo jana wakati akifunga mafunzo kwa walimu wa vyuo vikuu vitano katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Dk. Silima alisema endapo taaluma ya TEHAMA itatumika ipasavyo katika vyuo na madarasa mengine ya kujifunzia, itasaidia kurahisisha shughuli za ufundishaji.

Alibainisha kuwa kutokana na maendeleo ya TEHAMA duniani kote, vyuo vya kimataifa vina taratibu za kutoa baadhi ya maelezo na aina za video katika mitandao kupitia taaluma za kada mbalimbali za masomo, hivyo wanafunzi wanapaswa kuitumia fursa hiyo kujifunza.

Aidha, alisema matumizi ya TEHAMA yatasaidia kurahisisha utoaji elimu, hivyo walimu wana uwezo wa kufundisha zaidi ya darasa moja kwa vyuo tofauti na hatimaye kupata idadi kubwa ya wanafunzi.

Mkurugenzi huyo aliwataka walimu waliopatiwa mafunzo hayo kutumia mbinu za ufundishaji walizopatiwa ili kutoa elimu inayoendana na wakati kwa kundi kubwa la wanafunzi wa vyuo mbalimbali vya Zanzibar.

Alisema miradi ya TEHAMA imeacha athari Zanzibar kutokana na umuhimu wake kwenye kufundisha.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Elimu katika Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), Faith Shayo, alisema baadhi ya changamoto za maradhi yakiwamo ya UVIKO – 19, zimekuwa kikwazo katika kipindi kilichopita hali ambayo imeathiri suala la elimu.

Aliwataka walimu waliopata mafunzo kuyatumia kufundisha wanapokua mbali na chuo ili kuleta mabadiliko katika utendaji kazi na masuala yote yanayohusu elimu kutokana na teknolojia kukua kwa haraka.

Pia aliipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ushirikiano katika utekelezaji wa mradi huo kusaidiana kuwasisitiza wanafunzi kutumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya kujifunza vitu vya maana.



**IBRAAH**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE





# WANAOCHAPIA KIINGEREZA
## Diamond, Harmonize waongoza kwa wanamuziki

HIVI karibuni kumeibuka mjadala kuhusu baadhi wa wasanii nyota wa Muziki wa Bongo Fleva, kuzungumza vibaya lugha ya Kiingereza.

Wasanii wanaoongoza kukosolewa kila kukicha kuhusu matumizi sahihi ya lugha ya Kiingereza ni Diamond Platnumz na Harmonize.

Wanamuziki hao licha ya kutumia lugha ya kingereza kama njia muhimu ya kuwaunganisha na wenzao wa nje ya nchi, lakini wamekuwa wakitumia katika mazungumzo yao ya kila siku na mashabiki wao.

Iwe kwenye mahojiano au katika mitandao ya kijamii, Harmonize na Diamond, wamekuwa wakitumia lugha mbili yaani Kiswahili na Kingereza kwa wakati mmoja.

Hata hivyo, kutokana na kutoijua vyema lugha hiyo wamejikuta wakiandika maneno sio sahihi na kusababisha watu kuwashambulia.

Kwa mfano hivi karibuni, Harmonize, amejikuta yupo katika utata baada ya maelezo yake kwenye Instagram akieleza hali ya mahusiano aliyokuwa nayo akimlenga aliyekuwa mpenzi wake Kajala, kukosewa maandishi.

Kwenye maelezo hayo ametumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza, lakini kuna baadhi ya maneno ya kiingereza yamekosewa.

Kwa mfano ameandika 'Don't gev up on me' badala ya 'Don't give up on me', pia amesema 'Im sorry i known how i didi you wrong', alitakiwa kuandika 'Im sorry i know i did you wrong'.

Baadhi ya watu wamewashauri wasanii hao wakubwa kujifunza vizuri lugha hiyo kabla hawajaamua kuwa sehemu yao ya mawasiliano.

BASI SAWA

## Ibraah chunguza anaweza kuwa wako



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Ibraah Tz, amekana kuwa na mtoto na mwanamke anayefahamika kwa jina la Kim Mishepu.

Ibraah aamesema anakumbuka huko nyuma alikuwa na mtoto ambaye mama yake aliitwa Pendo, lakini alifariki dunia.

"Nakumbuka nilikuwa na mwanamke anaitwa Pendo huko Sinza, lakini huyu Kim Mishepu simjui na sina mtoto naye," amesema.

## Q Chief usiwafokee wenzako



MKONGWE wa muziki wa kizazi kipya, Q Chief haimuingii akilini kuona watu wanamfananisha Saraphina na Vanessa Mdee.

Q Chief anasema Saraphina anafanya vizuri kwa sasa lakini si kumfananisha na Vanessa kwani kila mtu ana heshima yake.

"Viatu vya mtu visivaliwe na mtu mwingine, yaani mnataka kumfananisha Saraphina na Vanessa Mdee kweli? anafanya vizuri kwenye game lakini tuheshimu kile tunachokiona kila siku" - Q Chief



## Marioo usiwe kama kipepeo

MKALI wa Bongo Fleva,Marioo anasema mahaba anayofanyiwa na mpenzi wake mpaka yanampa hofu.

Amesema mara nyingi anapofanya kitu kizuri mpenzi wake huwa anamtumia maua na ujumbe kumpongeza. Hata alipopata tuzo za TMA, alitumiwa maua na ujumbe mzuri wa kumpa moyo.

"Haya mahaba mwenzenu mpaka naogopa, hivi ndio vitu mzee wa bring back my family anavikosa" amesema Marioo.



## Hascana kama kweli wapo watakaokufuata

MUONGOZAJI bora wa video za muziki katika tuzo za Tanzania Music Awards 2021 (TMA), Hanscana, amesema mwili wake mdogo unatokana na kazi nyingi anazofanya.

Amesema sio kama hapendi kuwa na mwili bali kufanya kazi kwa bidii usiku na mchana kunamfanya asipate mwili kama wengine.

"Nafanya kazi kwa bidii sana. Si unaniona mimi sikui, nakonda unadhani sipendi kuwa na mwili ila nashuti kila siku ". amesema Hanscana

## WABONGO WALIOIGA STAILI YA FRANCO

**Na Adam Fungamwango**

WALA siyo siri kuwa muziki wa zamani Tanzania ulitawaliwa au kuathiriwa zaidi na staili ya upigaji kutoka Zaire (sasa Jamhuro ya Kidemokrasi ya Congo) na Congo Brazaville.

Kulikuwa na msururu wa bendi nyingi sana kwenye nchi hizo mbili na wanamuziki bora kabisa, kiasi cha bendi nyingi nchini kuiga nyimbo kwa mirindimo, huku wakibadilisha tu maneno.

Mfano wa hilo ni wimbo wa Kilwa Jazz, 'Napenda Nipate Lau Nafasi', ambao ni maarufu hadi leo.

Huu wimbo ni kama kopi tu ya wimbo wa 'Mokolo Nakukufa' ulioimbwa Tabu Ley Rochereau mwaka 1966.

Ni maneno yaliyobadilika pamoja na lugha, lakini jinsi unavyoimbwa na upigaji unafanana kabisa.

Huo ni mfano tu, zipo nyimbo nyingi sana kama hizo za Congo zilizobadlishwa na kuimbwa kwa lugha ya kishwahili na bendi za Tanzania miaka hiyo.

igaji wa kwanza uliitwa soukous wa pili uliitwa odemba.

Leo nitauzungumzia mtindo wa odemba. Ni staili iliyobuniwa na mfalme wa rhumba duniani, Luambo Luanzo Makiadi Franco.

Sikiliza nyimbo nyingi za Franco jinsi gita lake linavyolia, kama kwamba mtu anapiga chumba na si nyuzi.

Hapa Tanzania kuna wanamuziki wengi waliiga aina ya upigaji huo wa staili ya kente au mwenyewe aliita odemba.

**Mbaraka Mwinshehe Mwaruka**

Huyu si upigaji tu, kwani alimuiga Franco kwa kila kitu hadi kufuga ndevu. Na hata wajihi wao walifanana sana. Ukimuoa Mbaraka alikuwa amefanana sana na Franco.

Tukija kwenye muziki, wote wawili wanapiga magita ongozi ya solo na kuimba pia.

Mbaraka alimuiga Franco kwenye upigaji aina ya kente. Ukitaka kumsikia vizuri, sikiliza wimbo wa 'Benki ya Taifa ya Biashara' na 'Unanitafutia nini?'. Humo kuna kente la kufa mtu.

**Said Mabera**

Marehemu Said Mabera, aliyekuwa kiongozi wa bendi ya Msondo Ngoma Music, tangu wakati inaitwa Juwata Jazz.

Huyu nyimbo zake zote amepiga kwa staili hiyo ambayo Franco amekuwa akiipiga.

Lakini ukitaka kujua shughuli yake sikiliza vibao kama 'Faulata', 'Piga Ua Talaka Utatoa', 'Kalumanzira', na 'Ajali'. Unaweza ukazani kama anayepiga ni Franco mwenyewe.

**Shem Karenga**

Alikuwa ni kiongozi wa bendi ya Tabora Jazz wana Segere Matata. Marehemu Shem, naye alikuwa ni mtaalam wa upigaji wa gitaa la staili ya kente. Linasikika zaidi kwenye nyimbo kama 'Sarafina', 'Dada Asha', 'Dada Remmy', 'Halima', 'Chakula Kwa Jirani', na 'Farida'.

**Hamza Kalala**

Huyu naye ni mfuasi wa Franco. Karibuni nyimbo zake zote anapiga kwa mtindo wa odemba.

Msikilize kwenye nyimbo nyingi za Vijana Jazz, kama vile 'Amba', 'Madaraka Kwenye Baa', 'Stella', 'Tambiko la Pambamoto', 'Bujumbura' na nyingine nyingi alizopiga kwa mtindo huo.

**Shaaban Yohana 'Wanted'**

Huwezi kuwatajа wafuasi wa Franco hapa Bongo kama hujamtaja Wanted. Ni hatari kabisa. Msikie kwenye nyimbo za Vijana Jazz kama 'Heshima ya Mtu', 'Aza Umeniumbua' na nyingine nyingi.

## Danga la Uswazi: Lamdangia mume wa shoga 'ke

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU ya 'Danga la Uswazi' linaonyesha maisha halisi ya mtaani, hasa kule wanakoishi watu wengi, maarufu kama 'uswahilini'. Mara nyingi huko jamii inaishi pamoja, na kila mmoja anakuwa na mtazamo, tabia na akili zake.

Kutokana na kukutanika kwa watu kutoka sehemu tofauti, malezi tofauti na tabia pia, kunakuwa na vurumai na mambo mengi ambayo kwa mtu ambaye hajazoea kukaa uswazi yatakushangaza.

Hebu kidogo fuatilia filamu hii kama unakaa 'uzunguni' unaweza kushangaa, lakini kama uswazi au ulishawahi kuishi huko, unaweza tu kutabasamu na kukumbuka mengine ambayo umeshawahi kuyaona na kuyasikia.

Imechezwa na kina Sikudhani Mohamed, Emma Mkango, Janeth Kimambi, Habiba Timu, Shamim na wengineo.

Habiba anadaiwa pesa ya mchezo wa upatu kiasi cha shilingi elfu thelathini lakini hana pa kuzipata. Biashara yake ya machungwa haiwezi kumfanya kupata kiasi kicho kwa siku chache.

Kijumbe Feti anakuja kumdai kwa madai na yeye anasumbuliwa na watu 'wanaotoka', yaani wenye zamu ya kupewa hizo pesa. Zogo linakuwa kubwa na wanavurugana haswa. Feti anampa siku moja awe ameilipa.

Habiba anakutana na Mkango, mwanaume wa shoga yake ambao naye yupo kwenye huo upatu.

Mkango anamsifia Habiba, naye anaona ndiyo fursa ya kumdangia. Wanaelewana kukutana kwa shilingi elfu hamsini.

Kesho yake Habiba anaipeleka hiyo pesa kwa Feti. Lakini hakuondoka bila kumwambia alikoipata kwa kumdangia Mkango, mume wa shoga yao Sekela.

Siku chache baadaye Feti anakutana na Mkango. Utoaji pesa kwa Habiba, ulimtoa udenda. Akamuomba amkopeshe shilingi elfu hamsini. Mkango kama kawaida yake, samaki hapishi chambo. Wakakubaliana malipo. Lakini baada ya hitimisho, pesa haikutimia waliokubaliana. Feti ni mtoto wa mjini, akachukua pesa iliyokuwepo na simu juu.



Sekela, mke wa Mkango anapata nyepesi kuwa Habiba anatembea na mume wake, anamfuata huko huko na kuzusha timbwili. Nyumba sasa ikawa chungu kwa Mkambo na mkewe. Hakuliki wala hakulaliki.

Kwenye petroli kukawashwa moto, kwani siku ya kupokea pesa zake za upatu zilipofika, Seleka alienda kwa kijumbe Feti kuchukua pesa zake. Ikuwa ghafla sana. Feti hakuweza hata kuficha simu aliyoichukua kutoka kwa Mkango. Sekela akamuuliza alikoipata simu ya mumewe. Varangati likaanza. Sekela akawa na uhakika kuwa kumbe shoga zake, Feti na Habiba wanamdangia mumewe.

# Kim azidi kupagawa penzi jipya

MWANAMITINDO na mshiriki kipindi cha maisha cha TV, Kim Kardashian, amesema kwa sasa ana furaha na amani kuwa na mpenzi wake mpya Pete Davidson.

Mama huyo wa watoto wanne, amesema hayo wakati akihojiwa na runinga ya ABC katika kipindi chake cha "GMA" kinachoendeshwa na Robin Roberts.

"Ninamaanisha uhusiano wangu ni wa kipekee,nisingekuwa naye kama nisingepanga kufanya matanuzi kila wakati nikiwa naye. Hakika nina furaha na ninajihisi kuwa na amani zaidi," amesema.

Kim ameachana na mumewe wake rapa Kanye West hivi karibuni baada ya mahakama kuridhia wawili hao kila mmoja awe huru kufanya mambo yake.





## Rita, Anosike kufunga ndoa?

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Rita Dominic, anatarajia kuvunja ukimya kuhusu uhusiano wake wa kimapenzi na Fidelis Anosike.

Imeelezwa wawili hao wana mpango wa kuvishana pete ya uchumba kwa siri na kuishi pamoja.

Dominic na Anosike imeripotiwa kuwa watafunga ndoa katika jimbo la Imo April 18, mwaka huu.

## Card B apandisha mizuka

RAPA mkali wa Marekani, Cardi B, ameamua kufuta akaunti yake ya Twitter, baada ya jina lake kutotajwa miongoni mwa mastaa walioalikwa katika tuzo za Grammy.

Msanii huyo ambaye ni mama wa watoto wawili, kabla ya tukio hilo alikuwa na wakati mgumu baada ya wafuasi wake kumjia juu kuhusu mtoto wake.

"Nimefuta akaunti yangu ya Twitter, lakini Mugu wangu nawachukia wafuasi wa aina hii, hata hivyo kama naenda Grammy na kama siendi haiwahusu," ameandika Card B.





## Rihanna afurahia kuwa bilionea

MWANAMUZIKI kutika visiwa vya Barbado Rihanna, hatimaye amejiunga kundi la watu wanaojiita mabilionea.

Kulingana na jarida la Forbes, staa huyo mwenye miaka 34,ana utajiri unaofikia dola bilioni 1.7 mpaka sasa.

Forbes inaeleza katika utajiri wake, muziki haumuingizii kipato kikubwa, lakini pesa nyingi anapata katika biashara zake za nguo na urembo.

## Shatta ashambuliwa kwa kujiona

NYOTA wa muziki kutoka Nigeria, Shatta Wale amejikuta akikosa furaha baada ya watu kumfananisha na mwanamuziki chipukzi kutoka Ghana, Black Sherif.

Mwimbaji huyo wa Ghana mwenye umri wa miaka 20 ametoa wimbo mpya ambao umekuwa maarufu 'Kwaku The Traveller' na kuwafanya mastaa wa Nigeria kupagawa nao kiasi ambacho umekuwa namba moja katika chati za muziki nchini humo.

Wimbo huo umesababisha mashabiki wengine wazidi kumshambulia Shatta kutokana na tabia yake ya kujivuna lakini hajaweza kushika chati ya juu nchini Nigeria licha ya kutoa nyimbo 1000.



MAKALA

# Tanzania inapojizatiti kufikia uchumi wa kidijitali kwa kukamilisha mfumo wa anwani za makazi

Na Mary Geofrey




Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James akizindua anwani ya makazi katika wilaya yake.

ANWANI za Makazi ni mfumo unaotambulisha mahali halisi ambapo mtu anaishi, biashara au ofisi anayofanyia kazi.

Anwani ya makazi inatolewa kwa kufuata jina la barabara, mtaa, namba ya nyumba au jengo pamoja na Postikodi.

Postikodi au simbo za posta kama inavyotambulika, ni mfumo maalum wa tarakimu unaotambulisha eneo la kufikisha huduma za posta na kwa nchi ya Tanzania inaanzia katika ngazi ya kata, wilaya, mkoa na kanda.

Meneja wa Kitengo cha Huduma ya Posta, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Harune Lemanya, anasema serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatekeleza mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi nchini.

Anasema lengo ni kurahisisha mawasiliano, ufikishaji wa huduma za serikali kwa wananchi na kufanyika kwa shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutawala.

Anafafanua kuwa, kuna aina tatu kuu za anwani zinazotumika ulimwenguni ambazo ni anwani za kijiografia, anwani za posta na anwani za Makazi.

Lemanya anasema, anwani za Kijiografia ambazo huitwa pia anwani za maeneo hutumia mifumo ya urejeleaji kwa mfano longitudo na latitudo kutoa maelezo sahihi na ya kudumu ya mahali kitu kilipo duniani.

Anaeleza aina ya pili ni Anwani ya Posta hutumia taarifa za mahali halisi ili kufikisha bidhaa za kiposta au kifurushi.

Anwani ya makazi ambayo hutumia majina ya barabara na mitaa na namba za nyumba kuonyesha mahali sahihi pa kudumu na mahususi kitu kilipo mfano anwani za maeneo na milki.

Anasema anwani za makazi hutumia mfumo wa utambulisho wa barabara, mitaa, majina ya majengo, nambari za nyumba, kielelezo kama vile Postikodi.

Manufaa ya Anwani za Makazi

Anasema anwani za makazi zitaiwezesha nchi kufikika kirahisi.

Aidha, anasema itawawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa kidijitali, wataweza kufanya biashara kati yao na nje ya nchi kwa kuzingatia kuwa mizigo inaweza kutumwa pale mtu alipo au kutumiwa mzigo ukamfikia pale alipo.

Anasema mfumo wa anwani za makazi na Postikodi utawezesha kila raia kuwa na anwani halisi ya makazi tofauti na ilivyokuwa awali suala la anwani lilikuwa uchaguzi wa mtu binafsi.

**Anasema lengo la viwango vya mfumo wa anwani ni kuwasaidia watoa huduma za posta na huduma nyingine zikiwamo za dharura na biashara, kutoa huduma kwa ufanisi, usahihi na kwa wakati, hivyo kupunguza uwezekano wa hasara na upotevu wa namna yoyote uwe wa mali, muda au maisha na hatimae kumwezesha mpokeaji huduma kuipata bila vikwazo.**

Utaratibu huu wa Anwani za makazi kila biashara inayosajiliwa Tanzania itakuwa na anwani halisi, utambulisho wa watu wanaoishi nchini. Pia itarahisisha usajili wa mali, biashara, vizazi na vifo.

Utaboreshwa,huduma za dharura, kama vile polisi, zimamoto na magari ya wagonjwa, zitaweza kutambua maeneo yenye dharura na kuyafikia kwa haraka na urahisi zaidi.

“Wageni wataweza kubaini mahali wanakokwenda kwa urahisi zaidi badala ya kuuliza mara kwa mara uelekeo wa kule waendako,”anasema Lemanya.

Sababu za Anwani za makazi

Lemanya anasema uwekaji wa Anwani za makazi unalindwa na taratibu za Kimataifa ambazo zimeridhiwa na nchi wanachama wa Umoja wa Posta Duniani.

Anasema viwango stahiki vya uwekaji Anwani za makazi na Postikodi vinapaswa kuzingatiwa na nchi zote wanachama.

“Tanzania ina mwongozo wa mfumo wa anwani za makazi uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI, unaoelekeza hatua na taratibu za kufuatwa wakati wa uwekaji anwani za makazi nchini.

Hivyo viwango vya uwekaji huzingatia taratibu za Kimataifa na ki-nchi kwa kadri zinavyoelekeza,” anaongeza Lemanya.

Aidha, anasema viwango vya mfumo wa anwani wa Taifa vimewekwa kwa kuzingatia Mwongozo wa kiwango cha Kimataifa (S42) cha Umoja wa Posta Duniani (PAPU).

Anaeleza Umoja wa Posta Duniani ni Shirika la Umoja wa Mataifa lenye dhamana ya maendeleo ya sekta ya posta duniani, pia ni msingi wa ushirikiano baina ya watoaji wa huduma za posta duniani.

Umoja huu unasaidia kujenga mtandao wa uhakika duniani unaohakikisha utoaji wa huduma za kisasa za posta. Kwa njia hii, shirika linafanya kazi za kushauri, kupatanisha, na kutoa msaada wa kitaalamu kila upohitajika.

Anasema lengo la viwango vya mfumo wa anwani ni kuwasaidia watoa huduma za posta na huduma nyingine zikiwamo za dharura na biashara, kutoa huduma kwa ufanisi, usahihi na kwa wakati, hivyo kupunguza uwezekano wa hasara na upotevu wa namna yoyote uwe wa mali, muda au maisha na hatimae kumwezesha mpokeaji huduma kuipata bila vikwazo.

Viwango katika zoezi la anwani ni muhimu kwa kuwa vinarahisisha mawasiliano .Moja ya vipengele muhimu vya mafanikio ya uwekaji viwango katika zoezi la utoaji wa anwani ni Kuwezesha mawasiliano yenye mpangilio bora uliohifadhiwa.

**UTOAJI WA JINA LA BARABARA AU MTAA**

Lemanya anasisitiza ili kuipa majina mitaa au barabara, mtaa husika utashirikisha wadau wote wa eneo husika hususan wakazi wa eneo hilo.

“Suala la utoaji majina ya mitaa na barabara ni muhimu sana kuwa shirikishi kwa kuwa barabara ni miundombinu ya umma; Anwani za makazi ni suala linaloigusa jamii nzima” anaeleza Lemanya.

Kiongozi huyo, anasema utaratibu wa utoaji majina ya mitaa na barabara utaanzia katika ngazi ya mtaa, kitongoji na kuendelea katika ngazi ya kijiji, kamati ya maendeleo ya kata, kamati ya kudumu inayohusika na masuala ya mipango miji na mazingira na hatimaye Baraza la Madiwani.

Anasema mwongozo wa Anwani za Makazi umebainisha kuwa halmashauri itawajibika kutoa taarifa kwa wadau wote juu ya majina ya mitaa yaliyoidhinishwa na kuingizwa katika daftari la kudumu la majina ya barabara au mitaa katika halmashauri husika.

Katika mkutano kazi na wakuu wa mikoa uliofanyika Februari jijini Dodoma mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alisisitiza kuwa ni muhimu wananchi wakashirikishwa katika kila hatua ya mradi wa Anwani za makazi.

“Kwa hiyo tukiwashirikisha vizuri wananchi, hili zoezi litakwenda kuwa rahisi na halina ughali ule ambao tuliutarajia wa kitaalam” alisisitiza Rais Samia Suluhu.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James, anasema wilaya anayoiongoza inazingatia utaratibu unaotumika katika kupata majina ya mitaa kama ulivyobainishwa kwenye mwongozo na jina la mtaa litatoka kwa wananchi kupitia mkutano mkuu wa mtaa au kitongoji husika.

“Watu wengine wanaweza kuchagua jina la mtu kutokana na kusaidia jamii hiyo kama kujenga barabara na wakati huo huo na yeye kuwa mkazi wa mtaa au kitongoji,” anasisitiza James.

Shauku ya serikali awamu ya sita ni kuona mfumo wa anwani za makazi unakamilika ifikapo mwezi Mei 2022.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOELEKEA...

# Utoto zamani, kila nyumba kuna njiwa

## •Unawajua? dume, jike wanalalia mayai
## •Aina zao; Tz, Choki, kombokombo...

Na Adam Fungamwango

HIVI sasa imekuwa ni nadra sana kuona watoto kuanzia miaka saba, hadi 15 wakifuga wanyama au ndege, hasa wale wa mijini. Nasema mijini kwenye mikoa yote Tanzania, kwa sababu siku hizi hata mikoani, sehemu za mijini hazitofautiani sana mazingira ya maisha na Dar es Salaam.

Kwenye miaka ya 1970, 1980 hadi mwishoni wa 1990, kuanzia Dar es Salaama na baadhi ya mikoa, kulikuwa na fasheni ya watoto wengi kufuga njiwa.

Kama nilivyosema awali, watoto wa zamani walikuwa mahodari sana wa kufuga wanyama kama mbwa, sungura, kuku na bata, lakini moja kati ya mifugo iliyokuwa kivutio ilikuwa ni njiwa.

Kwa sababu ufugaji wake ulikuwa na mambo mengi sana, na ilikuwa ni sifa kwa mtoto, au kijana yoyote kuwa na njiwa nyumbani kwake, ingawa si wengi waliofanikiwa kuwafuga na kuwa nao moja kwa moja, kutokana na masharti yanayodaiwa kuwapo.

Masharti mengine yalikuwa ni ya kweli, lakini mengine ilikuwa ni dhana, pamoja na utamaduni wa sehemu husika.

Kwanza kabisa wafuga njiwa wote ni lazima wajuane. Na hii ilitokana na kwamba njiwa wana tabia ya kutembeleana, au kuhama sehemu moja kwenda nyingine, hadi mwenyewe atakapokwenda kuzungumza na mfugaji mwenzake ili kufanya utaratibu wa kuwarudisha.

Hii wenyewe waliita mateka. Na kama walikwenda mbali zaidi kwa mfugaji ambaye hawajuani ndiyo imeisha hivyo.

**NJIWA NI NDEGE WA AINA GANI?**

Njiwa ni ndege wanaopenda sana amani.Kimsingi njiwa hapendi usumbufu na kurushwa roho kwa vitisho. .Hawagombani kama ndege wengine wakati wa kula. Hutumika kama alama ya amani, mapenzi, matumaini na mshikamano.

Kama nilivyosema awali ni ndege wasiopenda fujo ukiwafuga kama ni nyumba iliyojaa ugomvi na vurugu, wanahama wote. Wanapenda kula mtama na kunde.

Na inashauriwa kabla ya kuwafuga ni lazima ufahamu masharti yao, ambayo mengine ni ya kweli na mengine ni dhana za kufikirika, lakini wafugaji wengi huyatekeleza.

Kwanza kabisa njiwa ukiwanunua kutoka kwa mtu, sharti wawe wawili 'pea', yaani dume na jike.

Kama muuzaji aliwafuga kwa banda la juu, mnunuzi ahakikishe anakowapeleka anawaandalia banda la juu, ukiwaweka la chini wanaondoka.

Kama banda lako la chini, ni lazima mnunuzi atafute muuzaji mwenye banda chini ndipo ununue vinginevyo unashauriwa uwanyonyoe manyoya na kuwafungia siku 40 kabla ya kuwafungulia.



Njiwa hawapendi makelele ya kushtukiza kama honi kali, kuwarushia jiwe na miziki mikubwa, ukifanya hivyo wanahama.

Inasemekana njiwa wana mapenzi ya kweli na wana wivu baada ya nyegele, hivyo mfugaji ni lazima ahakikishe anawafuga wawili wawili.

Inadaiwa pia kuwa njiwa ndio viumbe pekee duniani wenye mpenzi mmoja, yaani huyo mmoja akipotea au kufa anayebakia huendelea kuomboleza kifo cha mpenzi wake, hadi atakapotafutiwa mwingine, naye atakuwa ni huyo tena pekee.

Kama mmoja akifa, inashauriwa atafutiwe mwezake na kama haikuwa hivyo, aliyebaki ataondoka.

Ukimfuga njiwa hata akiruka umbali gani hasahau nyumbani lazima arudi, labda awe ametibuliwa kwa sababu mbalimbali, ndiyo ataenda kwa wenzake wanaofugwa na wengine ambao wanawaita mateka.

Ndiyo maana toka zama hizo, hata waimbaji na wanatunzi wa nyimbo wanamuimba njiwa kama mpeleka salamu sehemu fulani hasa kwa mpenzi, kwa sababu ni lazima atarudi kurejesha ujumbe.

Faida ya kufuga njiwa inatajwa kuwa ni urembo, burudani, kitowewo na baraka.

**TABIA, DHANA, TAMADUNI ZA WAFUGAJI**

Kuna dhana ambazo hazijafanyiwa utafiti wowote, lakini zimekuwa zikiaminiwa sana wa wafugaji wa ndege huyo.

Nazo ni kwamba eti wakiwa mbele yako usipende kuwajadili kwa sababu hawapendi masimango, la sivyo wataondoka.

Kuna imani kuwa hawapendi mfugaji awe mmbeya na mwenye kusengenya watu, au mlevi, lakini pia hawataki anayewamiliki awe na tabia chafu na za kishirikina, au kama mwanaume anagombana na mkewe mara kwa mara, au mumewe, ikiwa pia kugombana majirani wanaweza kuondoka. Hizi ni dhana na utamaduni ambao wafugaji wanautilia sana maanani, na ndiyo maana wafuga njiwa wengi ambao huwafuga kwa ufanisi zaidi hadi kupata njiwa wengi, ni watoto zaidi kwa sababu hawana mambo mengi kama hayo.

Pia inasemekana hawapendi kuona wenzao wanachinjwa mbele yao, watahama wote kwa sababu wanahisi utawachinja.

Sasa kali zaidi kuna hii, eti hata kama msiba, au watu wengi wamekusanyika nyumbani ambapo wanafugwa ni lazima mfugaji wakati anawapa chakula awaambie kuwa kuna tatizo, labda ni msiba, sherehe, mkutano au chochote kile kilichowafanya watu wawe wengi, la sivyo wanaweza kuhama. Hizi ni dhana na utamaduni wa wafuga njiwa.



**KUFAHAMU, JIKE AU DUME**

Wafuga njiwa wote wanakubaliana kuwa ili kumtambua jike au dume kuna vitu itakakiwa vifanywe na kuangaliwa.

Njiwa dume huwa na kifua kipana na umbo kubwa, na ukimshika mdomo kwa kumning'iniza mbawa zake zinapapalika, au kupigapiga, hapo utajua kuwa ni dume, lakini jike ukifanya hivyo yeye hapapaliki.

Njiwa jike hutaga mayai mawili, na jukumu la kulalia au kuatamia ni la wote wawili, dume na jike ambao hufanyiana zamu.

"Njiwa wangu, walipoanza kuokota majani yakiwa ni maandalizi ya kutaga, jike akakanyagwa na gari na kufa. Akabaki dume peke yake. Sasa hili dume, lilikuwa lina tabia ya kutoka pale nyumbani, na kwenda mbali nisikokujua. Baada ya siku chache, akaja na jike, alikompata, hata sijui.

Baada ya siku chache, hilo jike likataga mayai mawili. Baadaye nikapata vifaranga. Kabla hawajaanza kuruka vizuri, wakataga tena. Sasa, kilichoniudhi, na kuchukia kuwafuga hao ndege, ni tabia iliyokuwa nayo hilo dume. Pamoja na kuwa nilijenga mabanda mengi, lakini watoto wake wakianza kuruka vizuri tu, alikuwa anaondoka nao, na kuwaacha huko huko. Kwa hiyo muda mrefu, nilikuwa nina vifaranga tu, wakikua, wanahamishwa. Nikagundua kuwa kumbe walikuwa wakienda kule alikomtoa mama yao." Ni maneno aliyoyasema kijana mmoja mfugaji aliyekuwa akiwafuga.

**MAJINA YAO**

Njiwa wana majina kama watu vile. Na majina hayo wanabuniwa na watoto, ambao ndiyo wafugaji wakubwa.

Hapa nchini kila njiwa anatambuliwa kwa jina fulani kutokana na rangi aliyonayo, au manyoya miguuni, na mengine yanayofanana na hayo.

Hakuna kikao rasmi cha watoto ambacho kilikaa kuwapa majina, ila kokote utakakokwenda utakuta wanaitwa majina hayo hayo, ambayo si halisi, ila ya kuwatunga wenyewe.

Mwenye manyoya meupe anaitwa sanaa, halafu yule mwenye manyoya miguuni, wanamwita masoksi.

Kuna manyota ambao wana mabaka ya rangi nyeusi na nyeupe, mashanga wao wana baka jeupe kichwani. Majina mengine ni kombokombo, chokichoki, choki maziwa, na TZ, ambaye ni maarufu sana, kwani njiwa wengi nchini wana rangi hiyo, ambayo ni ya kahawia na mabaka meusi.

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Russia yashambulia kituo cha treni

## ●Watoto wa Putin wazidi kubanwa




Kituo cha treni kilichoshambuliwa na kombora, watu wengi walikuwa hapo wakikimbia mashambulizi ya Russia Mashariki mwa Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

NCHI ya Uingereza imeungana na Marekani kwa kuwawekea vikwazo mabinti wawili wa Rais wa Russia Vladimir Putin.

Mabinti hao wanafahamika kwa majina ya Katerina na Maria Vladimirov, wameingizwa rasmi kwenye orodha ya vikwazo vya Uingereza.

Vikwazo walivyowekewa watoto hao ni sehemu ya juhudi zilizoratibiwa na Marekani ambayo tayari imeweka vikwazo.

Serikali ya Uingereza pia iliamua kumuwekea vikwazo binti wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov, anayefahamika kwa jina la Yekaterina Sergeyev.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari ya Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza ilisema inalenga zaidi maisha ya kifahari ya watu wa karibu wa Putin, na kwamba wamepiga marufuku ya kusafiri na kufungia mali kwa watatu hao.

Kwa mujibu wa serikali ya Uingereza, zaidi ya paundi 75 bilioni ya kitengo cha vita cha Putin sasa imehifadhiwa na vikwazo vilivyoratibiwa vya Uingereza na kimataifa katika wiki za hivi karibuni.

Iliongeza kuwa Russia inaelekea kwenye mdororo mkubwa zaidi wa uchumi tangu kuporomoka kwa Umoja wa Kisovieti huku vikwazo vikiathiri uwezo wa Rais Putin wa kuanzisha vita nchini Ukraine.

**WATU 30 WAUAWA KITUO CHA TRENI**

Katika hatua nyingine, Kampuni ya Reli inayomilikiwa na serikali iliripoti kuwa, watu 30 waliuawa na wengine zaidi ya 100 kujeruhiwa katika shambulio la roketi la Russia kwenye kituo cha treni cha Kramatorsk.

Kramatorsk kilikuwa mojawapo ya stesheni za mashariki ambazo bado zinaendelea kufanya kazi nchini Ukraine na Gavana wa Donetsk, alisema maelfu ya watu walikuwa kituoni hapo wakati huo wakijaribu kupanda treni.

Mkuu wa reli ya Ukraine, alisema roketi mbili zilipiga kituo hicho.

Mwenyekiti wa Shirika la Reli la Ukraine, Oleksandr Kamyshin, katika ujumbe wake kwa njia ya Telegram, aliandika kwamba, kituo cha treni katika jiji la Kramatorsk huko Donetsk kimepigwa kwa makombora na kwamba watu kadhaa wameathirika.

Halmashauri ya jiji la Kramatorsk iliwaonya watu kukaa kwenye makazi yao.

Kramatorsk ilijulikana kuwa mojawapo ya njia kuu za uokoaji kutoka Mashariki mwa Ukraine.

**Peskov alikanusha pendekezo lolote kwamba wanajeshi wa Russia walihusika na mauaji katika mji wa Bucha na kuliambia shirika la utangazaji kwamba, wanaishi katika siku za kughushi na uwongo.**

Wanajeshi wa Russia ni janga kubwa

Russia imekiri kupata hasara kubwa ya wanajeshi nchini Ukraine, huku uvamizi huo ukiingia siku yake ya 44.

Msemaji wa Rais Putin, Dmitry Peskov, alikiambia Kituo cha Uingereza cha Sky News kuwa waliopoteza maisha ni janga kubwa kwao.

Alisema anatumai Russia itafikia malengo yake ya vita katika siku zijazo. Maoni ya Peskov yalifuatia kutimuliwa kwa Russia katika Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa siku ya Jumatano.

Wajumbe 93 kati ya 193 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, walipiga kura kuunga mkono karipio hilo la kidiplomasia, lililofuatia madai ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaofanywa na wanajeshi wa Russia katika mji uliokuwa unakaliwa kwa mabavu wa Bucha Kaskazini mwa Ukraine.

Hata hivyo, Russia ilitangaza kujiuzulu kutoka kwa baraza hilo wakati inajibu.

Chombo hicho kilionyesha wasiwasi wake kuhusu mzozo unaoendelea wa haki za binadamu.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky,aliishutumu Russia kwa ukatili zaidi huko Borodyanka, mji ulio karibu na Mji Mkuu wa Kyiv.

Peskov alikanusha pendekezo lolote kwamba wanajeshi wa Russia walihusika na mauaji katika mji wa Bucha na kuliambia shirika la utangazaji kwamba, wanaishi katika siku za kughushi na uwongo.

Alidai bila msingi wowote kuwa picha za raia waliouawa katika mji huo zilizoonyeshwa ni za kughushi.

Lakini hatua yake ya kukiri kwamba Russia imepata hasara ni kitendo cha kushangaza.

Machi 25 mwaka huu, Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema wanajeshi wake 1,351 waliuawa katika mapigano.

Ukraine imekadiria vifo vya Warusi kuwa ni takribani 19,000.

Hata hivyo, siyo Russia wala Ukraine makadirio ya hasara yanaweza kuthibitishwa. Wachambuzi wametahadharisha kuwa Russia inaweza kuwa inapunguza kiwango chake cha waathirika, wakati Ukraine inaweza kuiongeza ili kuongeza ari yake.

Viongozi wa nchi za Magharibi wanaamini kuwa kati ya wanajeshi 7,000 na 15,000 wa Urusi wameuawa.

**WANAJESHI WA RUSSIA WAZIDI KUONDOKA**

Wizara ya Ulinzi Uingereza ilisema, wanajeshi wa Russia walijiondoa kikamilifu kutoka Kaskazini mwa Ukraine, wakirejea kaskazini mwa Belarus na Russia.

Baadhi ya vitengo hivyo vitahamishiwa mashariki mwa Ukraine kupigana huko Donbas. Lakini vikosi vingi vitahitaji kuletwa kabla ya kutumwa.

"Usafirishaji wowote wa wanajeshi wengi kutoka Kaskazini kuna uwezekano kuchukua angalau wiki moja," wizara ilisema katika taarifa yake ya jana asubuhi.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa, mashambulizi ya makombora ya Russia katika miji ya Mashariki na Kusini mwa Ukraine yanaendelea na wanajeshi wa Russia wamesonga mbele Kusini kutoka Mji muhimu wa kimkakati wa Izyum.

BBC

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**JOACHIM MICHAEL PASIPANOFU** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 131468** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2019. Muda wake wa kuisha matumizi ni tarehe 2029. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye.

**TAARIFA YA POLISI: DAR/MAG/RB/140413/2022.**

## KUPOTEA KWA CHA CHETI



**HAPPY ADAM** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0259-0048** kilichotolewa na Baraza La Mitihani La Taifa kupitia shule ya sekondari SAMARITANI GIRLS SECNDARY SCHOOL CENTRE mwaka 2010. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ILO/RB/713/2012**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MANGI MTEMI RAMADHANI,** anatangaza kupotelewa na Cheti cha kidato cha Nne Index no **S.0800/0116** Kilichotolewa na baraza la mitihani katika shule ya **SECONDARY LOYALA** high school MWAKA 2018, yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote Polisi.

TAARIFA YA POLISI **DOD/DOD/RB/139063/2022**

**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) ARUSHA-ARUSHA**

**MAOMBI MADOGO NA. 366 YA 2021**

**MASAI LOBIKIEKI..........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**LOOTHA LOBUKA............................ MJIBU MAOMBI**

**KWA: LOOTHA LOBUKA...... POPOTE ULIPO**

**MASAI LOBIKIEKI,** amefungua shauri hili mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Arusha. Shauri husika limepangwa kutajwa mbele ya Mh. G. Kagaruki, Mwenyekiti tarehe 14/04/2022 saa tatu kamili asubuhi. Hivyo basi,unatakiwa kuhudhuria siku hiyo wewe au wakili wako au mtu yeyote utakayempa maelekezo juu ya shauri hili. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande moja na Uamuzi kutolewa dhidi yako pasipo wewe kusikilizwa. Nakala ya maombi haya inapatikana Ofisi za Baraza zilizopo katika Jengo la Mkuu wa wilaya Arusha.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 14 mwezi Machi, Mwaka 2022.

tarehe

MWENYEKITI

**IN THE DISTRICT COURT OF NJOMBE AT NJOMBE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 03 OF 2022**

**in the matter of estate of the late ............THOBIAS JOHN BMBILINYI**

**And**

**In the matter of application for LETTER OF ADMINISTRATION BY...............METHOD MBILINYI**

**GENERAL CITATION**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cite to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letters of administration) is made to the above named petitioner

Objections to the grant should filed on or before the 28th day of APRIL 2022

Dated at NJOMBE this 06 day of APRIL 2022

RESIDENT MAGISTRATE

## TAARIFA KWA UMMA

**MBAZI HERY SANGIWA WA P.O.BOX 543 ARUSHA**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA **NO 17201 ,PLOT NO 82 CORRIDO ARUSHA** MJINI. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **ARU/ARU/RB/124993/2022.**

## KUPOTEA KWA KADIYA GARI

Ndugu **KASHUMARI SWAIBU HASSAN** amepoteza kadi ya gari namba **T667 DHP** aina ya Nissan Extrail .Taarifa ya kupotea kwa kadi imetoewa katika kituo cha Polisi Muleba RB namba **KAG/MUL/484989/2021.** Atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

## JOB OPPORTUNITY TRANSPAPER (T) LIMITED

Has a vacancy in **IMPORTS DEPARTMENT.**
**Education:** A graduate in procurement and logistics management or in accountancy with minimum3 years' experience.
Send your Application at **info@transpaper.co.tz**
**Mobile: 0684626364**

## KUPOTEA KWA KADI YAPIKIPIKI

**MAWENGE BACHELEMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya SANLG yenye usajili namba MC 750 **CFD yenye CHASSIS NAMBA LBRSPJB58K9002432 ,** namba ya kadi **SL157FM119901634.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: GE/RB/1765/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MONICA JOSPER LWENJE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T914BVU** aina ya **TOYOTA CAMI,** Chassis No. **J122E0088781,** Engine No. **K30943810.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya **Polisi.DOD/DOD/RB/137983/2022**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-21

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

Kwa mbali miguu ilianza kumchezacheza Jan. Alikuwa amekaa kwenye kochi kwa muda mrefu bila kuongea, wala kuingilia maongezi hayo.

Wakati anafunguliwa geti na kuingia, Diana alimwambia Jan asiongee chochote kile na yeye atamaliza kila kitu.

Kama kuna kitu alitaka kuongea, lakini akasita.

"Utaua wangapi ndugu yangu?"

"Ina maana Diana una wanaume wengi kiasi kwamba unaniambia utaua wangapi?"

"Sina mwanaume, ila tu sitaki kuwa na wewe, mwanaume usiyejua kupenda. Watu wananihangaikia usiku na mchana, wewe unastarehe tu huko na wanawake wengine. Mwenyewe unaona umenidanganya kusema ulisafiri, mimi habari zako zote ziko hapa." Diana alisema huku mkono wake wa kulia ukipiga mkono wa kushoto.

Baada ya maneno ya kuudhi, kejeli na dharau kuzidi, Challa akaamua ni bora tu aondoke.

"Mimi naondoka. Lakini kuondoka kwangu siyo kama yameisha. Ni lazima nione mwisho wake. Muda mfupi huu umetoka lakini umekuwa na jeuri na kiburi. Nina uwezo na pesa za kupeleleza kujua nani anakupa kiburi chote hiki. Na mimi nitadili naye."

"Dili na mimi kwanza, muone vile, hebu ondoka kwetu, na hapa iwe mwanzo na mwisho kukanyaga."

***************************

"Tunamfanyaje sasa mtu huyu?" Jan aliuliza. "Maana tukimuachia atatusumbua na anaweza kutufanya tusiwe na raha."

"Usiwe na wasiwasi Jan, unakumbuka nilikwambia zamani kabla sijatekwa kuwa hili niachie mimi? Ukawa na wivu kwa marehemu afande Marco na Challa?"

"Nakumbuka, na wakati ule nilijua huenda baadaye ukanizingua tu, wala sikukuamini sana."

"Basi sasa ndiyo uamini, nilikuwa na maana yangu, nitakwambia baadaye. Ila kwa sasa wewe mpigie simu mkuu wa kituo cha Polisi Magomeni, si unafahamiana naye uliongea naye siku ile nilipookolewa?"

"Nakumbuka mpenzi."

"Mwambie kuna mtu katutishia. Mimi nadhani huu ndiyo muda muafaka wa kuwa na wewe na si tena kuwa na watu wengine tofauti, huku wewe ukiwa kivuli chao. Nataka niwe na wewe pekee, tujiachie. Mmoja ameshakwenda ambaye ni afande Marco, huyu anatushinda nini?" Diana aliongea kwa msisitizo, akimpa ushauri Jan.




**"Kwani wewe na Diana ndiyo kwanza mmekuwa wapenzi? Halafu si nasikia huyo msichana alikuwa na uhusiano na afande mwenzetu marehemu afande Marco?"**

"Naam, umeongea kitu." Jan alisema huku akitoa simu yake ya mkononi mfukoni na kumpigia Mkuu.

"Naam kijana, umenikumbuka leo, vipi kwema huko?"

"Kamanda kwema, lakini si sana."

"Kwa nini?"

"Kuna mtu mmoja anaitwa Challa, anatusumbua sana na mpenzi wangu, huyu ambaye mlimuokoa majuzi."

"Mwambie anaitwa Dickson Challa." Diana alimnong'oneza Jan.

"Nani umesema?" Mkuu wa Kituo aliuliza.

"Anaitwa Dickson Challa, huyu jamaa amekuja nyumbani hapa na kututishia maisha."

"Kwa nini amefanya hivyo?"

"Afande ni kwamba zamani alikuwa mpenzi wa Diana, lakini kwa sasa wameachana, sasa anamtishia, na pia anasema akigundua mpenzi wake mpya, basi atamfanyia kitu kibaya."

"Kwani wewe na Diana ndiyo kwanza mmekuwa wapenzi? Halafu si nasikia huyo msichana alikuwa na uhusiano na afande mwenzetu marehemu afande Marco?"

"Afande ni hadithi ndefu kidogo."

"Najua lakini, sisi maafande tunajua mengi kuliko nyinyi raia, inavyoonekana huyo mpenzi wake, alikuwa na wapenzi watatu kwa wakati mmoja. Ndiyo maana wewe na afande Marco mlipambana ili kumuokoa, sasa inawezekana huyo naye ameshatoka, sasa anamtaka, na kwa mwanamke jinsi alivyo hawezi kuwa na mtu ambaye hajachangia chochote kwenye kuokoa uhai wake." Kamanda aliongea kama mtu anayejua kila kitu, kiasi cha kumshangaza Jan.

Kabla hajajibu lolote, kamanda akaongeza tena "Sawa, wewe kesho njoo kituoni hapa Magomeni ili uandikishe maelezo, tuanze hiyo kazi, sawa?"

"Nitashukuru afande."

********************************

Ilikuwa ni furaha kubwa. Furaha isiyomithilika, baina ya Jan na Diana. Walikuwa wamekaa kwenye kochi kama wapenzi halisi.

Mjomba Ken alipita na kuwaangalia. Akatabasamu.

"Mpwa wangu, sasa umepata mchumba. Tayari nina barua yako. Huyu ni mtu sahihi kwako kwa sababu alikuwa bega kwa bega wakati ule umetekwa. Alinifundisha mambo mengi na ujanja mwingi. Ndiyo nikajua kweli huyu ni mtoto wa mjini. Tulikuwa hatuna pesa ya kukukomboa, lakini alifanya kila njia kupata angalau kianzio, na mipango mingine ya kimjini mjini ili mradi tu urudi nyumbani salama. Ni yeye ndiye aliyejitoa mhanga kwenda kuweka mkoba wa pesa usiku wa manane sehemu zote mbili ambazo watekaji walituambia. Daraja la Mfugale na mara ya pili Kajima, bila kujali uhai wake. Kusema kweli Jan anakupenda sana Diana na mimi nimeamini hivyo na sina kipingamizi kama akiwa mumeo. Utakuwa umepata mume bora. Na kama mkioana, mimi nitawapa ile nyumba ya Tabata, iwe yenu."

Maneno hayo yalitoka kinywani mwa mjomba wake Diana, Ken ambaye alikuwa amesimama na baada ya hapo alipita na kwenda chumbani kwake.

Jan na Diana walitazamana kwa huba. Penzi kuonekana zaidi kuliko kusikika. Kila alichokiongea Ken kilikuwa sahihi.

Ghafla waliacha kuangaliana. Ni baada ya televisheni iliyokuwa mbele yao kuonyesha picha ya Dickson Challa akiwa mikononi mwa polisi.

Taarifa ilisema kuwa mmiliki wa kampuni ya kusambaza mbolea nchini Dickson Challa ametiwa mikononi mwa polisi kutokana na makosa mbalimbali, ikiwemo kutishia, pamoja na uhujumu uchumi.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Kinondoni ni kwamba, mtuhumiwa aliwauzia wakulima mbolea iliyokuwa chini ya viwango, kitu ambacho kimewasababishia hasara wakulima wengi nchini, ambapo ni sawa na kuhujumu uchumi wa nchi.

Kosa la pili ni kuwatishia kuwaua, raia wema wawili ambao majina yake yamehifadhiwa kwa sasa. "Tuko salama sasa mpenzi." Diana alinong'ona kwa furaha. Jan hakujibu kitu. Furaha ilizidi kiasi cha kushindwa kuongea chochote.

"Kumbuka, nilikwambia suburi Jan. Lengo langu lilikuwa ni kupata mwanaume sahihi, kati yenu, afande Marco, Challa na wewe. Nilikwambia muda ndiyo utaongea. Leo hii natamka wewe ndiyo mwanaume bora kwangu na nimekubali uwe mume wangu."

Maneno hayo yalikuwa yakijirudia kama mwangwi kwenye sikio la Jan. Kila akifikiria mara ya kwanza alipokutana na Diana kule Mwananyamala na kumsaidia kutoka kwa yule kibaka aliyempora mkoba kwenye pesa, haamini kuwa mrembo yule ambaye hata mwenyewe alikuwa akimuogopa kutokana na uzuri na urembo wake, wakati yeye ni fukara, lakini leo yuko mikononi mwake. Ni kama ndoto nzuri aliyoota ambayo imekuja kuwa kweli.

**MWISHO**

# SIMBA YALIA KUKOSA MABAO MENGI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA msaidizi wa Simba, Selemani Matola akiri kuwa wamekuwa wakikosa mabao mengi kwenye mechi mbalimbali wanazocheza, huku wakiwa wanetengeneza nafasi nyingi za kufunga.

Akizungumza juzi mara baada ya kukamilika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union, Matola amesema kuwa wamekuwa wakilifanyia kazi sana suala hilo kwenye uwanja wa mazoezi, lakini anaona bado linajirudia, hivyo bado wana kazi ya kufanya.

Simba ilibidi isubiri dakika za majeruhi kuweza kupata bao la pili likifungwa na Meddie Kagere, na kupata ushindi wa 2-1 kwenye Uwanja wa Mkwakwani, mjini Tanga.

"Mechi haikuwa rahisi, ukicheza na Coastal Union ikiwa kwao, lazima utegemee kuwa mechi hiyo itakuwa ngumu. Niwapongeze tu wachezaji wangu, wamepambana hadi mwisho na kupata bao licha ya kukosa mabao mengi, hasa kipindi cha pili. Nasema hivyo kwa sababu tumetengeneza nafasi nne au tano, lakini hatukuzitumia, ingawa suala hili tumekuwa tukilifanyia kazi sana kwenye uwanja wa mazoezi. Lakini tutaendelea kurekebisha ili kupata mabao mengi kwenye mechi, kwa sababu tunatengeneza nafasi nyingi, ila kuzitumia tu ndiyo tatizo," alisema Matola, kiungo mkabaji na nahodha wa zamani wa timu hiyo.

Naye kocha Mkuu wa Coastal, Juma Mgunda ambaye ilikuwa ni mechi yake ya kwanza tangu arejee kukinoa kikosi hicho alisema soka ni mchezo wa makosa, na uchanga wa wachezaji wake ulisababisha kufanya makosa ya kujirudia ambayo wapinzani wao waliwaadhibu.

"Ukifanya makosa ya kujirudia kwenye timu na wachezaji wenye uzoefu kama Simba ni lazima watakuadhibu tu. Angalia, kuna mchezaji wangu mmoja, dakika zimeisha, akawa anataka kukokota mpira kutoka nusu ya kwetu hadi kwenye nusu ya timu pinzani wakati ameshachoka, akanyang'anywa mpira, ikapigwa ndefu, wakapata bao la pili. Lakini ni makosa yanayorekebishika, mimi nina siku nne tu tangu niichukue timu, nitayafanyia kazi. Kikubwa tu niwapongeze wachezaji wangu kwa kujituma, wamepambana na mwisho wa siku ni lazima tukubali matokeo," alisema Mgunda, straika wa zamani wa timu hiyo.




Ben Pol (kulia) akitoa burudani kwenye uzinduzi wa SYP. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ben Pol atoa neno uzinduzi wa SYP

**Na Sabato Kasika**

MSANII nyota wa muziki wa kizazi kipya Benard Paul Mnyang'anga 'Ben Pol', amesema anajivunia kujitolea kwa nguvu na kutumia muda wake katika uhifadhi wa mazingira kama shujaa wa Umoja wa Mataifa wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's).

Pol alisema hayo wiki hii katika uzinduzi wa mpango wa kuboresha na kuimarisha ustawi na maendeleo ya vijana na vijana balehe kwenye maeneo ya afya, elimu, ushiriki, ushirikishwaji na uwezeshaji kiuchumi uitwao Safeguard Youth People Programme (SYP).

SYP inatekelezwa na ufadhili wa Ubalozi wa Uswisi nchini kupitia Shirika la Swiss Development Cooperation kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania.

"Pamoja na kazi ya muziki ninayoifanya, mimi ni balozi wa mazingira na ninaendelea kutunga nyimbo mbalimbali za kuhamasisha utunzaji wa mazingira nchini ili Tanzania iendelee kuwa ya kijani kibichi," amesema 'Ben Pol'.

Alisema amekuwa balozi anayeheshimika wa uhifadhi wa mazingira wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumfanya kupata mialiko mbalimbali ukiwamo huo wa uzinduzi wa SYP.

'Ben Pol' amesema jukumu lake ni kuongeza uelewa kwa watu kuhusu kufufua upya mazingira ya kijani kibichi kwa kuhamasisha upandaji miti na kushughulikia suala la mabadiliko ya hali ya hewa.

Aidha, alisema yeye ni miongoni mwa wale wanaopenda kutembelea mbuga za wanyama hasa za Serengeti ili kufanya utalii, kwa madai kwamba, mbuga hiyo ina maeneo mengi ya kuvutia.

"Unaweza ukawa Serengeti ukajiona upo Manyara, mandhari tofauti na ina idadi kubwa ya wanyama ikilinganishwa na mbuga nyingine, hivyo ninapenda sana kutembelea mbuga ya Serengeti," amesema.

## Simba Queens kuja kivingine

**Na Saada Akida**

KOCHA MKUU wa Simba Queens, Sebastian Nkoma amesema mzunguko wa pili wanakuja kivingine kuhakikisha wanaendelea kuvuna pointi katika michezo 11 ya duru hilo la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkoma alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo chanya katika michezo iliyopo mbele yao kuhakikisha wanatetea taji la ubingwa wa ligi hiyo.

Alisema kwa sasa anaimarisha kikosi chake kwa sababu amekuwa na upungufu wa wachezaji na baadhi yao kuondoka kwa sababu mbalimbali ikiwamo kucheza soka la kulipwa nje ya nchi na wengine kujiunga na jeshi.

"Tumerejea kambini kuhakikisha tunazidi kuimarika zaidi ya mzunguko wa kwanza na kuhakikisha tunapambana kutafuta matokeo chanya kila mechi ili kufikia malengo yetu ya kumaliza ligi bila ya kupoteza," alisema kocha huyo.

Simba Queens inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 33 ikishinda michezo yote 11 ya mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo ya wanawake.

## Chilunda kukaa nje wiki nne

**Na Saada Akida**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Shaban Chilunda anatarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa wiki nne baada ya kupata majeraha ya goti na kutarajiwa kufanya mazoezi Juni 6, mwaka huu.

Chilunda alipata majeraha ya goti wakati timu hiyo ilipokuwa na mechi ya kirafiki na DTB FC, wakijiandaa dhidi ya Yanga, mchezo uliopigwa juzi Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, daktari wa Azam, Mwanandi Mwankemwa alisema nyota huyo alifanyiwa vipimo vya MRI kutoka na majeruhi hili, Hospitali ya Orthopaedic Surgeon Vicente Palloti, mjini Cape Town, Afrika Kusini.

Alisema baada ya kufanyiwa vipimo hivyo amegundulika kupata madhara ya kuumia mtulinga (Ligament) wa Kati-Pembeni na kutakiwa kupumzika kwa wiki nne.

"Daktari Robert Nicolas anamfanyia uchunguzi amethibitisha Chilunda hana haja ya kufanyiwa upasuaji lakini anatakiwa akae nje ya Uwanja kwa takribani wiki nne baada ya hapo ataanza kufanya mazoezi mapesi na atakuwa amepona kabisa," alisema Mwankemwa.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE NA KITITA
KLABU ya Paris St-Germain imempatia mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, kitita cha euro milioni 150 kwa misimu miwili ili abaki klabuni hapo. ***(Guillem Balague)***

### PHILLIPS ATAKIWA MAN
MANCHESTER United inashughulikia kumsajili kiungo mwingine wa kati wa England na Leeds United, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26. ***(Manchester Evening News)***

### GUARDIOLA KUPEWA BRAZIL
BRAZIL inajiandaa kumpatia kocha wa Manchester City, Pep Guardiola donge nono ili awe kocha wa timu yao ya taifa**.** ***(Marca)***

### LAMPARD AUNGWA MKONO
KOCHA wa Everton, Frank Lampard anaungwa mkono na mmiliki wa klabu hiyo, Farhad Moshiri na bodi ya klabu ya Goodison Park, licha ya Toffees hao kukaa pointi moja tu juu ya eneo la kushuka daraja. ***(Mail)***

### AWONIYI AWINDWA
NEWCASTLE United na West Ham zina mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Union Berlin na Nigeria , Taiwo Awoniyi mwenye umri wa miaka 24 msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### KONSA AWANIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal inamuwinda mlinzi wa Aston Villa na England, Ezri Konsa mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

### NEVES KUMRITHI PALHINHA
KLABU ya Wolves imemuona kiungo wa kati wa Sporting Lisbon na Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 26, kuwa anafaa ikiwa Ruben Neves akaondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(GiveMeSport)***

### BEI YA NUNEZ YATAJWA
ARSENAL, Manchester United na Tottenham Hotspur zimeambiwa kuwa zinahitajika kulipa pauni milioni 67 ikiwa zitataka kumsajili mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22 kutoka Benfica. ***(Express)***

### NKETIAH AGOMBEWA
LEEDS United na Brighton wanataka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 22. ***(Ekrem Konur - Fichajes)***

### GVARDIOL AWINDWA
MLINZI wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20 anawindwa na Tottenham Hotspur. ***(Athletic)***

### BISSOUMA KUPEWA MKATABA
ASTON Villa imeonesha nia ya kumpatia mkataba kiungo wa kati wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND AIKATAA MAN UNITED

Asema akitua Old Trafford malengo yake hayataweza kufikiwa, Man City waongoza kwenye mbio za kuipata saini yake na...

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland ameripotiwa kukataa ofa yoyote kutoka kwa Manchester United msimu huu kwa sababu ya hofu kwamba Mashetani Wekundu hao 'hawawezi kufikia malengo yake'.

Mshambuliaji huyo ambaye anayehitajika zaidi duniani kwa sasa amekataa kuhamia Old Trafford wakati akitarajiwa kuondoka Borussia Dortmund msimu huu wa joto.

Haaland, ambaye ana kipengele cha kununuliwa kwa pauni milioni 63, anasakwa na klabu kadhaa kubwa barani Ulaya baada ya kufunga mabao 80 katika mechi 83 akiwa na wababe hao wa Bundesliga tangu awasili kutoka Red Bull Salzburg Januari, 2020.

Manchester City wanaripotiwa kuwa tayari kumfanya raia huyo wa Norway kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi nchini England, kama ilivyobainishwa na Sportsmail mwezi uliopita, na mabingwa hao wa Ligi Kuu ndio walio mstari wa mbele katika kinyang'anyiro cha kumsaka nyota huyo mwenye umri wa miaka 21.

Lakini inaonekana hatahamia Old Trafford msimu huu wa joto, licha ya kuhusishwa sana nao alipojiunga na Dortmund kwa sababu ya kuhusishwa na makocha wa zamani, Ole Gunnar Solskjaer.

Kwa mujibu ESPN, wawakilishi wa Haaland wamewafahamisha United kwamba hatahamia huko kwa sababu anahisi "hawawezi kuendana na matarajio yake".

United, ambao wanakaribia kufikia makubaliano ya kumchukua kocha wa Ajax, Erik ten Hag msimu huu wa joto, wanasaka sana mshambuliaji mpya msimu huu wa joto.

Inadaiwa kuwa Mashetani Wekundu wameifahamisha kambi ya Haaland kwamba watakuwa tayari kufikia ofa yoyote ya fedha ili kuipiku Man City au mtu mwingine yeyote anayevutiwa na mchezaji huyo.

Lakini wawakilishi wa raia huyo wa Norway waliiambia United kwamba ubora wa 'mradi wa michezo' utakuja kwanza na uamuzi wa Haaland hautatokana na manufaa ya kifedha.

Man City na Real Madrid - zote zinashindana mara kwa mara kuwania mataji yao ya nyumbani na katika hatua za mwisho za Ligi ya Mabingwa Ulaya – na ndio wanaonekana kuwa kwenye mtali wa mbele kuwania saini yake.

Haaland pia anasemekana kuwa na hamu ya kuendelea na maendeleo yake na anahisi mchezo wake utapanda viwango vipya chini ya kocha Pep Guardiola.

Mtendaji Mkuu wa Dortmund, Hans-Joachim Watzke alidai wiki iliyopita kwamba ofa yoyote ambayo Man City itawasilisha kwa Haaland haiwezi kufikiwa kwa upande wa Bundesliga.

Masuala ya kibinafsi yamejadiliwa na viongozi hao wa Ligi Kuu huku Haaland akitarajiwa kuwa mchezaji anayelipwa zaidi kwenye Ligi, akiwa na mshahara unaozidi pauni 500,000 kwa wiki.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,119

MECHI KALI
EVERTON
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 4.04
X | 3.61
2 | 1.83

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RICE KUWEKA REKODI YA USAJILI



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ipo tayari kuvunja rekodi yao ya uhamisho wa kumnasa Declan Rice na kumfanya kuwa usajili wao mkuu kipindi cha majira ya joto ya kwanza chini ya kocha mpya, Erik ten Hag, kwa mujibu wa 90Min.

Rice ameibuka kuwa mmoja wa viungo chipukizi bora zaidi barani Ulaya na ndiye nguzo muhimu kwa West Ham United ambayo imetinga hatua ya kumaliza nne bora msimu huu.

90min anaelewa kuwa Rice na wawakilishi wake wameweka wazi kwa West Ham wanaona mwaka huu ni wakati mwafaka kwake kusonga mbele na kuendeleza kipaji chake sehemu nyingine.

West Ham walikuwa wameanzisha mazungumzo kuhusu mkataba mpya wa mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwaka jana, ingawa klabu hiyo inajua kwamba hawataweza kufikia mishahara anauotaka.

Inatarajiwa kwamba Rice ataweza kuweka mfukoni angalau pauni 250,000 kwa wiki tofauti na ule anaolipwa kule kwa wagonga nyungo.

David Moyes alipendekeza wiki iliyopita kwamba ingechukua pauni milioni 150 kumnunua Rice, lakini vyanzo vilivyo karibu vimethibitisha kwamba, mtu anayekaribia pauni milioni 120 atamwona mkuu wa Wagonga nyundo David Sullivan akiidhinisha uhamisho huo.

Pia ajirani wa Manchester City na wapinzani wa ligi Chelsea nao wanatajwa kuwania saini ya mchezaji huo.

Awali Liverpool walikuwa wameonesha nia ya kutaka kumnunua Rice mwaka jana, lakini gharama ya jumla ya mkataba huo inaonekana kuwaweka kando.

# Xavi aipania Eintracht Camp Nou

**MUNICH, Ujerumani**

XAVI alitoa wito kwa mashabiki wa Barcelona kuifanya Camp Nou "jiko la shinikizo" baada ya kutoka sare ya 1-1 dhidi ya Eintracht Frankfurt katika mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Europa.

Ansgar Knauff aliipatia Eintracht bao la kuongoza kwa kumalizia vyema mapema kipindi cha pili kwenye Uwanja wa Deutsche Bank Park Alhamisi, lakini Ferran Torres alisawazisha baada ya kazi nzuri ya Frenkie de Jong.

Timu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ilishuhudia Tuta akitolewa nje kwa kadi nyekundu zikiwa zimesalia zaidi ya dakika 10, lakini Barca hawakuweza kupachika bao la ushindi katika hatua za mwisho.


Xavi alihisi kuwa timu yake ilitatizwa na hali ya uwanja na anatumaini hali ya hewa nzuri kule Katalunya kwenye mchezo wa pili a Alhamisi ijayo inaweza kusaidia Blaugrana hao kutinga nusu fainali.

"Walikuwa wapinzani sana. Walisonga mbele kwa kasi. Hatukuwa na mzunguko wa mpira na hali ya uwanja haikutusaidia," alisema Xavi akiiambia Movistar mara baada ya mchezo huo.

"Tunaondoka tumeridhika kabisa na Camp Nou itabidi iwe jiko la shinikizo, kama ilivyokuwa kwenye uwanja wao.

"Hatukuweza kusimamisha mashambulizi yao. Tulikuwa tayari tumeonywa - waliiondoa timu kama (Real) Betis (katika 16 bora)."

Gerard Pique alitoka nje katika kipindi cha kwanza baada ya kuumia, lakini Xavi hakuweza kutoa taarifa za maana kuhusu mlinzi huyo wa kati.



## HABARI MICHEZO

,012,860

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/04/22 | 17:00 | Watford vs Leeds | 2.75 | 3.29 | 2.49 |
| 02. 09/04/22 | 17:00 | Preston vs QPR | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 09/04/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.63 | 3.13 | 2.63 |
| 04. 09/04/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Union Berlin | 2.69 | 3.19 | 2.59 |
| 05. 09/04/22 | 20:00 | Amiens vs Bastia | 2.63 | 2.93 | 2.78 |
| 06. 10/04/22 | 15:15 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.37 | 3.48 | 2.73 |
| 07. 10/04/22 | 16:00 | Sivasspor vs Basaksehir | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 10/04/22 | 16:00 | Brentford vs West Ham | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 10/04/22 | 16:00 | Norwich City vs Burnley | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 10. 10/04/22 | 16:00 | Brest vs Nantes | 2.43 | 3.22 | 2.92 |
| 11. 10/04/22 | 17:15 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.78 | 3.13 | 2.63 |
| 12. 10/04/22 | 17:30 | St. Gallen vs FC Basel | 2.39 | 3.53 | 2.68 |
| 13. 10/04/22 | 20:00 | Strasbourg vs Lyon | 2.60 | 3.30 | 2.65 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 09/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1510 | St. Pauli vs Werder Bremen | 2.67 | 3.56 | 2.35 |
| 14:30 | 3730 | Schalke 04 vs Heidenheim | 1.79 | 3.71 | 3.96 |
| 14:30 | 5061 | Everton vs Manchester Utd | 4.04 | 3.61 | 1.83 |
| 14:45 | 3748 | Sheffield Utd vs Bournemouth | 2.30 | 3.23 | 2.98 |
| 15:00 | 1828 | Lecce vs Spal | 1.54 | 3.92 | 5.75 |
| 15:00 | 2011 | Cadiz CF vs Betis | 3.28 | 3.18 | 2.27 |
| 15:00 | 5601 | Alessandria vs Pordenone | 1.71 | 3.47 | 4.86 |
| 16:00 | 2295 | Caykur Rizespor vs Konyaspor | 3.49 | 3.49 | 1.99 |
| 16:00 | 2726 | Goeztepe vs Kayserispor | 2.11 | 3.54 | 3.14 |
| 16:00 | 3510 | Empoli vs Spezia | 1.96 | 3.55 | 3.60 |
| 16:30 | 1450 | Greuther Furth vs Monchengladbach | 4.49 | 3.99 | 1.68 |
| 16:30 | 1633 | FC Koln vs Mainz | 2.41 | 3.30 | 2.85 |
| 16:30 | 2065 | VfL Wolfsburg vs Arminia Bielefeld | 1.66 | 3.75 | 5.00 |
| 16:30 | 2600 | Bayern Munchen vs Augsburg | 1.12 | 8.97 | 15.95 |
| 16:30 | 5955 | Rubin Kazan vs FC Krasnodar | 2.68 | 3.28 | 2.48 |
| 17:00 | 1201 | Preston vs QPR | 2.19 | 3.21 | 3.21 |
| 17:00 | 1746 | Southampton vs Chelsea | 3.80 | 3.55 | 1.90 |
| 17:00 | 2077 | Millwall vs Barnsley | 1.72 | 3.42 | 4.86 |
| 17:00 | 2936 | Dundee Utd vs Dundee FC | 2.15 | 3.23 | 3.33 |
| 17:00 | 3117 | Celtic vs St Johnstone | 1.12 | 7.37 | 19.91 |
| 17:00 | 3285 | Swansea vs Derby | 2.06 | 3.22 | 3.52 |
| 17:00 | 3390 | Blackburn vs Blackpool | 1.71 | 3.57 | 4.66 |
| 17:00 | 3782 | West Bromwich vs Stoke City | 1.89 | 3.36 | 3.95 |
| 17:00 | 4027 | Bristol City vs Peterborough | 1.76 | 3.67 | 4.16 |
| 17:00 | 4094 | Livingston vs Motherwell | 2.13 | 3.08 | 3.58 |
| 17:00 | 4255 | Middlesbrough vs Hull City | 1.55 | 3.91 | 5.54 |
| 17:00 | 4749 | Watford vs Leeds | 2.60 | 3.40 | 2.55 |
| 17:00 | 5212 | Nottingham vs Birmingham | 1.61 | 3.70 | 5.33 |
| 17:00 | 5247 | Reading vs Cardiff | 2.31 | 3.12 | 3.07 |
| 17:00 | 5284 | Arsenal vs Brighton | 1.69 | 3.63 | 4.96 |
| 17:15 | 1833 | Frosinone vs Cremonese | 2.48 | 3.08 | 2.83 |
| 17:15 | 5231 | Mallorca vs Atletico Madrid | 4.15 | 3.29 | 1.94 |
| 18:00 | 2137 | Reims vs Rennes | 4.32 | 3.46 | 1.84 |
| 19:00 | 3238 | Inter vs Verona | 1.36 | 5.00 | 7.40 |
| 19:00 | 3247 | BSC Young Boys vs Lausanne-Sport | 1.29 | 5.59 | 8.38 |
| 19:30 | 1532 | Aston Villa vs Tottenham | 3.05 | 3.40 | 2.23 |
| 19:30 | 4196 | Hertha BSC vs Union Berlin | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 19:30 | 5741 | Villarreal vs Athletic Bilbao | 2.30 | 3.33 | 3.08 |
| 19:30 | 5858 | Akhmat Grozny vs Zenit St Petersburg | 4.45 | 3.70 | 1.71 |
| 19:45 | 4663 | Utrecht vs Fortuna Sittard | 1.49 | 4.37 | 5.56 |
| 20:00 | 2224 | Benfica vs Belenenses | 1.17 | 6.79 | 13.98 |
| 20:30 | 1125 | Besiktas vs Alanyaspor | 1.85 | 3.69 | 3.79 |
| 20:30 | 5837 | Gaziantep BB vs Trabzonspor | 3.19 | 3.34 | 2.16 |
| 21:00 | 4821 | Ajax vs Sparta Rotterdam | 1.07 | 9.92 | 21.82 |
| 21:30 | 4166 | Grasshoppers vs FC Luzern | 2.26 | 3.34 | 2.99 |
| 21:45 | 4537 | Cagliari vs Juventus | 5.16 | 3.68 | 1.65 |
| 22:00 | 1900 | Real Madrid vs Getafe | 1.47 | 4.15 | 7.17 |
| 22:00 | 2701 | NEC Nijmegen vs Twente | 3.81 | 3.46 | 1.89 |
| 22:00 | 4959 | Clermont Foot vs Paris St Germain | 7.25 | 5.02 | 1.37 |
| 22:30 | 2739 | Tondela vs Sporting Lisbon | 8.58 | 4.89 | 1.33 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# YANGA, GEITA GOLD ZAWINDANA FA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kimeingia kambini jana kujiandaa na mechi ya Kombe la FA dhidi ya Geita Gold Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huku wapinzani wao wakipiga kambi mjini Morogoro kwa ajili ya mechi hiyo ya robo fainali.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli amesema kuwa baada ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex na kushinda mabao 2-1, kikosi cha timu hiyo kumerejea kambini Ijumaa kujiandaa na mechi hiyo ambayo wanatarajia itakuwa ngumu.

"Tumeingia kambini, tunajiandaa na Geita Gold, tunajua wako Morogoro na tunafahamu mchezo utakuwa mgumu kwa sababu waliifunga Mbeya City kwenye mechi ya Ligi Kuu kwa hiyo watataka kujitutumua, lakini sisi tunawaambia Yanga tuna shida na hilo kombe la FA. Makocha wetu wanaelewa kuwa mechi hizi siyo kama za ligi, ni mtoano na makocha wanajua kuzicheza mechi kama hizi," alisema Bumbuli.

Kwa upande wa Geita Gold, Kocha Mkuu, Fred Felix Minziro amekiri ni kweli wameweka kambi mjini Morogoro kujiandaa na mechi hiyo.

"Baada ya kutoka kucheza dhidi ya Mbeya tumeamua kuweka kambi Morogoro, suala la lini tutakuja Dar tunaliacha na viongozi, ila nisema kuwa mechi itakuwa nzuri, unajua hii ni robo fainali na kila timu inataka kwenda nusu fainali. Mashabiki watarajie kuona burudani nzuri kwa kweli," alisema Minziro ambaye ni mchezaji na kocha wa zamani wa Yanga.

Yanga iliingia hatua hiyo kwa kuichapa Biashara United mabao 2-1, huku Geita Gold ikiidungua Mbuni kwa bao 1-0.



Bendi TPDF ya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), ikitumbuiza wakati wa maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 28 ya mauaji ya Kimbari nchini Rwanda yaliyotokea mwaka 1994 katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maua Sama atoa shukrani kwa Mungu

**Na Sabato Kasika**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Maua Sama amezungumzia wimbo wake mpya wa 'Shukrani' kuwa unalenga kumshukuru Mungu kwa kumjalia kuendelea kufanya vizuri katika muziki huo bila kukata tamaa.

"Nimempa shukrani Mungu wangu kwa matendo yake makuu kwangu, ndiyo maana nikatoa wimbo wa "Shukurani" ambao nimeimba katika vionjo vya RnB na Bongo Fleva," amesema Maua Sama.

Kimwana huyo alisema hayo hivi karibuni, kwenye hafla ya kutoa tuzo za Malkia wa Nguvu 2022 jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki alipokuwa miongoni mwa wasanii walioalikwa kutoa burudani.

Amesema, muziki huo una changamoto nyingi ambazo wakati mwingine zinaweza kukatisha tamaa na kurudishwa nyuma, na kwamba kwa nguvu ya Mungu yeye ameendelea kusimama imara.

"Ukweli nikitazama nilikotoka na nilipo sasa ni wazi Mungu amenibariki sana, sina budi kumshukuru, kwani wale ambao walitamani nikwame, wameshindwa kwa jina la Mungu aliye hai," amesema.

Msanii amesema, Mungu ameendelea kumfungulia milango na kumwezesha kufanya sanaa bila vikwazo njiani, kwa madai kuwa kila anachomuomba huwa anamtimizia na kwamba ataendelea kumtegemea.

Michezo

Jumamosi Aprili 9, 2022

Nipashe



## Haaland aikataa Man United




Kiungo wa Barcelona, Pedro Gonzalez Lopez maarufu zaidi kama Pedri (kulia) akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Frankfurt wakati wa mchezo wa kwanza wa robo fainali ya kombe la Ligi ya Europa baina ya timu hizo, Alhamisi usiku. Timu hizo zilifungana bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# KOCHA AL AHLY AIONYA ORLANDO KWA SIMBA

### Ni kwenye robo fainali ya CAF, huku VAR ikitumika kwa mara ya kwanza kwa Mkapa, mashabiki 60 waruhusiwa, Watunisia kuamua mechi ...

**Na Dennis Fussi**

KOCHA msaidizi wa zamani wa Klabu ya Al Ahly ya nchini Misri, Cavin Johnson amesema kwamba, timu ya Orlando Pirates itakabiliwa na wakati mgumu mno itakapocheza na Simba kwenye hatua ya robo fainali ya kombe la Shirikisho Afrika, CAF, huku kwa mara ya kwanza Tanzania itatumia VAR kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na mashabiki 60,000 wameruhusiwa kushuhudia.

Simba imepangwa kucheza na Pirates kwenye hatua hiyo baada ya kuitoa US Gendamarie ya Niger kwa ushindi wa 4-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam.

Kwenye mchezo huu mwamuzi wa kati atakuwa ni Haythem Guirat kutoka Tunisia, akisaidiwa na mwamuziki msaidizi namba moja, Khalil Hassani (Tunisia), mwamuzi namba mbili Samuel Pwadutakam (Nigeria) na mwamuzi wa akiba ni Sadok Selmi (Tunisia).

Mwamuzi wa teknolojia ya usaidizi kwa njia ya video (VAR) atakuwa ni Ahmed Alghandour (Misri) na msaidizi wake ni Youssef Elbosaty (Misri) na hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuitumia.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari wa Afrika Kusini, Johnson amesema itakuwa vigumu sana kwa Pirates na sio kitu rahisi kwao baada ya kupangwa na Simba kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

"Simba ni timu nzuri na inayosafiri sana, ina uzoefu wa kutosha na ni timu kubwa sana Tanzania," alisema Johnson akiwaambia wanahabari.

"Kuikabili Simba nyumbani kwao ni ngumu sana, sijui ni watu elfu ngapi watakuwepo uwanjani kuwashuhudia.

"Lakini mara ya mwisho nilikuwa pale na Al Ahly kulikuwa na mashabiki 30,000 hadi 40,000 uwanjani, hivyo utakuwa mchezo mgumu sana kwa Pirates nchini Tanzania na wanatakiwa kujiandaa vilivyo kuwakabili," aliongeza kocha huyo.

Simba iliichapa Al Ahly bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ikiwa chini ya Kocha Mkuu wa sasa raia wa Afrika Kusini Pitso Mosimane akisaidiwa na Johnson kwenye mechi ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Februari 23, 2021.

Lilikuwa ni bao la raia wa Msumbiji, Luis Miquissone, ambalo lilimpa moja kwa moja tiketi ya kusajiliwa na klabu hiyo ambao ni Mabingwa wa Afrika kwa sasa.

Ulikuwa ni msimu ambao Simba iliongoza kundi A, ikiwa na pointi 13, ikifuatiwa na Al Ahly ambayo ilimaliza ikiwa na pointi 11, AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo pointi saba na Al Merrikh ya Sudan iliyomaliza na pointi mbili.

Johnson mwenye umri wa miaka 63 raia wa Afrika Kusini, amewahi pia kuwa kocha mkuu wa timu za Platinum Stars (mara mbili), SuperSport United, Amazulu na Black Leopards (zote za Afrika Kusini).

Oktoba mwaka 2020, aliteuliwa kuwa kocha msaidizi wa Al Ahly chini ya Pitso Mosimane ambako alidumu hadi mwaka 2021.

Simba itaanzia nyumbani Aprili 17, kabla ya kusafiri kwenda Houghton Jijini Johannesburg kwa mchezo wa marudiano Aprili 24.

## Yanga SC sasa hakuna kulala

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umewataka wachezaji kutoridhika kwani bado safari yao ni ndefu ya kuhakikisha wanafikia malengo waliyojiwekea katika Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho la soka Tanzania (FA), msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya usajili ya Yanga, Hersi Said amesema wachezaji wanatakiwa kujituma zaidi na kutoridhishwa na matokeo wanayopata katika michezo yao 19 ya Ligi Kuu.

Alisema hawajapoteza mechi na malengo yao ni kuendelea kupata matokeo na ana imani kwa hali waliyofikia bado wapo kwenye safari ndefu zaidi ya walipotoka.

"Tunashukuru tumefanikiwa kufanya vizuri katika michezo 19 hatujapoteza, wachezaji hawatakiwi kuridhika haraka kwa sababu tunapokwenda ni kugumu na tuko katika safari ndefu ya kufikia malengo yetu," alisema Hersi.

Alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha msimu huu wanatwaa ubingwa wa ligi hiyo ambao wameukosa kwa misimu mitano mfululizo pamoja na taji la kombe la Shirikisho (FA).

Kwa upande wake, kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amesema amekuwa akiwasisitiza wachezaji kujituma na kufuata maelekezo anayowapa kuhakikisha wanafanikia malengo yao.

Alisema baada ya kumaliza michezo 19 na sasa wanatakiwa kuwa makini katika mzunguko wa pili kuhakikisha wanafikia malengo yao ya msimu huu ya kutwaa ubingwa wa ligi na FA.

"Wachezaji wanatakiwa kuwa makini kwa sababu mechi zilizobaki kwa sasa zote ni kama fainali na kila mmoja anatakiwa kutimiza majukumu yake ipasavyo akiwa uwanjani," alisema Nabi.

Alisema kwa wanaelekeza nguvu zao kwa mchezo wa robo fainali ya kombe la FA dhidi ya Geita Gold FC, kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Tumemaliza mechi na Azam FC na sasa tunajiaandaa dhidi ya Geita Gold FC, tunafanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa wapinzani wetu kuhakikisha tunapata matokeo mazuri na kucheza nusu fainali ya FA.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >